

MABWANA, SISI

TUNATAKA KUMWONA YESU

 ...usiku wa leo, huku Bloomington. Nimetazamia kuja huku kwa miaka miwili iliyopita. Nimekuwa nikijisikia kuongozwa kuja katika sehemu hii ya nchi, ambako nasikia ya kwamba wengi wa wainjilisti hawajawahi kuwa hapa, baadhi ya wainjilisti mashuhuri sana wa hili taifa hawajawahi kuingia katika nchi hii. Nami nilifikiri lingekuwa ni jambo kuu, nilipohisi mvuto wa Roho Mtakatifu kuja kuhudumu pamoja na hawa ndugu hizi siku nane usiku hapa, katika Jina la Bwana, kuja na kuingiza sehemu yetu ya juya, ili kuwavua watu. Na hiyo ndiyo kazi yetu hapa, ni kujaribu kuhakikisha Kanisa la Mungu linaongezeka katika nguvu Zake, na katika washirika Wake, na kwa utukufu wa Ufalme wa Mungu.

² Halafu basi, tunawaombea wagonjwa, hiyo ni sehemu ya Injili kama vile Bwana wetu Yesu alivyotuambia kwamba inatupasa kwenda ulimwenguni kote na kuihubiri Injili, na kuwaombea wagonjwa. Nasi tuna siku hizi usiku katika uamsho wetu ambapo tunawaombea wagonjwa. Hatudai kuwa mponyaji sasa, tunadai tu kwamba tunawaombea wagonjwa, kama mtu mwingine yeyote afanyavyo.

³ Tunaamini ya kwamba yote ambayo Mungu anaweza kuwafanyia tayari yamenunuliwa kwa ajili yenu pale Kalvari. Alipokufa pale Kalvari alimalizia ule mpango wa wokovu, ukombozi wa nafsi na mwili. Na sasa tunapata Arabuni ya wokovu wetu, ambayo ni Roho Mtakatifu, na halafu pia tuna A—Arabuni ya kufufuka kwetu, hiyo ni kusema, kwamba wakati miili yetu ni migonjwa, Mungu ndiye Mponyaji wetu. Ninaamini ya kwamba ni juu ya kazi iliyomalizika ambayo ilikamilishwa pale Kalvari, miaka elfu moja mia tisa iliyopita, wakati Kristo alipokufa kwa ajili yetu apate kutukomboha na mambo haya.

⁴ Siamini ya kwamba kuna mtu yeyote ambaye angeweza kusamehe dhambi, isipokuwa iwe ni dhambi dhidi yao. Kama ulikuwa umenitendea dhambi, halafu uniombe nikusamehe, ningeweza kufanya hivyo, na ningefanya hivyo. Lakini ninaamini kwamba, dhambi ambazo umementendea Mungu, kwamba Mungu Ndiye pekee anayeweza kusamehe dhambi hizo.

⁵ Pia ninaamini ya kwamba uponyaji wa Kiungu umewekewa msingi juu ya imani, kama tu wokovu, kwamba tunaamini ya kwamba alijeruhiwa kwa makosa yetu, kwa kupigwa Kwake sisi tuliponywa. Mnaona mtume Petro analiweka katika wakati

uliopita, “*Tuliponywa*.” Ni wakati uliopita, kama tu vile wokovu ni wakati uliopita. Wakati Yesu alipokufa pale Kalvari, aliuko ulimwengu mzima. Kila mwanadamu, ambaye angewahi kuwa duniani, swali la dhambi lilitatuliwa mara moja tu wakati Yesu alipokufa. Lakini kamwe, kamwe hutakuwa mrithi wa hati hii mpaka uikubali.

⁶ Wala hakuna kitu unachoweza kufanya kuistahili, ni jambo lisilostahilika ambalo Mungu amekufanyia. Nawe unalikubali tu kwa imani, katika urahisi wa imani Mungu amelifanya kusudi sote tuweze kulifikia. Tajiri au maskini, asiye na elimu au mwenye elimu, sote tunaweza kulikubali kwa sababu sisi sote tunaweza kulifikia, kwa urahisi tu kama wa mtoto kuamini ya kwamba “Ile kazi iliyomalizika pale Kalvari ilinijumuisha mimi.”

⁷ Vivyo hivyo na uponyaji wa Kiungu ambapo tunaamini ya kwamba uponyaji wa Kiungu ni kitu ambacho Kristo alitununulia pale Kalvari, ni bidhaa iliyomalizika ya Mungu, na jambo pekee tunalofanya ni kuipokea kwa imani, kuiamini. Hiyo ndiyo sababu tunaiita, “kuponywa kwa imani,” kwa sababu hivyo ndivyo ilivyo. Kwa hiyo isingeweza kuwa katika mtu binafsi, ati mtu yeyote kuwa na kitu *fulani* ambacho kingemponya mtu mwingine.

⁸ Kwa kweli, hakuna kitu kinachoweza kukuponya nje ya Mungu, “Mimi ni Bwana niponyaye magonjwa yako yote.” Maandiko hayawezi kukosea na hayawezi kuvunjwa. Basi, kwa hiyo dawa hazidai kuponya. Dawa, hatupingi dawa, dawa ni ya Bwana. Lakini dawa haiwezi kuponya, dawa inaweza tu—inaweza tu kusaidia maumbile katika mpango wa Kiungu wa Mungu wa uponyaji. Hakujakuwako na dawa iliyowahi kumponya mtu yeyote, hakuna daktari atakayekwambia hilo.

⁹ Kwa sababu, nilihojiwa kule Mayo Brothers siku moja, wakati *Reader's Digest* ilipoandika makala ile ya *Mwujiza wa Donny Morton*. Na kwenye hayo mahojiano, walisema, “Hatudai kuwa waponyaji, Bw. Branham, tunakiri tu kuyasaidia maumbile. Kuna Mponyaji mmoja, huyo ni Mungu.”

¹⁰ Kwa mfano, kama nilivunja mkono wangu, nikamwendea daktari, na kusema, “Ewe mponyaji mkuu, uponye mkono wangu, sina budi kuendeleza kazi yangu.”

¹¹ Mbona, angesema, “Unahitaji uponyaji wa akili.” Hiyo ni kweli, kama ningetoa tamshi kama hilo. Sasa, anaweza kuurudisha, kwa taaluma yake ya kisayansi anaweza kuurudisha huo mkono, bali hawezi kuuponya huo mkono, kwa sababu uponyaji ni ujumlishaji wa seli, na huo anaweza tu kufanywa na uhai pamoja na Mungu; Mungu ni uhai.

¹² Na kama nikiukata mkono wangu, halafu nikaanguka chini nikafa, huenda wakautia dawa mkono wangu uliokatwa, wangeweza kunidunga sindano za penisilini, na, miaka baada ya

miaka, wala huo usingepona kamwe. Kama wangeweza kuutia mwili wangu dawa usioze kunifanya nionekane wa kawaida kwa muda wa miaka hamsini, ningesema, usingepona, kwa sababu hakuna uweza wa uponyaji katika dawa, dawa huua tu kijidudu na kuudumisha safi huku Mungu akiuponya. Mnaona?

¹³ Sasa, dawa ilitengenezwa... Mara nyingi nimesema kwamba dawa ambayo ingeponya jeraha mkononi mwangu, ingeponya moja kwenye koti langu. Basi mtu fulani angesema, "Vema, sasa ngoja kidogo, dawa haikutengenezewa koti lako, ilitengenezewa mwili wako."

¹⁴ Vema basi, mbona haiponyi basi, baada ya uhai kutoka humo? Mbona haiponyi basi, kama ni kwa ajili ya mwili? Unaona? Ingefanya uponyaji kama huo *pale*, kadiri ingefanya *hapa*, kama ilikuwa ni kwa ajili ya mwili, ingeuponya huo mwili.

¹⁵ Lakini mnasema, "Vema, uhai huo hauna budi kuwepo." Hiyo ni kweli, kwa hiyo basi uhai ni Mungu, na Mungu ndiye Mponyaji. Mnaona? Kwa hiyo yote inarudi nyuma moja kwa moja, Mungu ndiye Mponyaji.

¹⁶ Maandiko hayajipingi Yenyewe. Wala hakuna Maandiko katika Biblia yanayojipinga Yenyewe; nimeomba nionyeshe hilo kwa miaka na miaka. Hakuna Maandiko, hakuna tamshi linaloweza kujipinga, pasipo kuweza kunyoshwa kwa Neno lingine la Mungu kuliweka pamoja vizuri. Ambapo Yesu alimshukuru Mungu, kwamba lilifichwa wenye hekima na akili, na lingefunuliwa watoto wachanga ambao wangejifunza. Mnaona? Sasa, hatuna budi kuwa wanyenyekevu katika jambo hili, hatuna budi kutupilia mbali mawazo yetu kulihusu, hatuna budi kukubali mpango wa Mungu wa jambo hilo, hiyo ndiyo njia pekee utakayoweza kufika popote pamoja na Mungu kwa ajili ya wokovu wa nafsi au mwili, itabidi ije kupitia mpango ulioandaliwa na Mungu.

¹⁷ Sasa, kama una kisima cha chemchemi upande *huu* wa mlima, kinachobubujisha mamilioni ya galloni za maji kwa saa, huku mimea upande wa pili inanyauka ipate maji, sasa, ungeweza kusimama na kupiga mayowe mpaka tezi za kooni zikupasukie, na ungeninii... na kupiga mayowe, "Loo, enyi maji makuu, njoni hapa mwimwagilie maji mimea yangu," hayataimwagilia, la, bwana, yatakaa papo hapo, lakini kama utafanya kazi kulingana na kanuni za uvutano, na kuyaelekeza maji haya yauzunguke huo mlima na kuimwagilia mimea yako, yataimwagilia, kama utafanya kazi kulingana na hizo kanuni.

¹⁸ Sasa, kuna umeme wa kutosha humu chumbani kukiangaza chumba, kama ulikuwa sawa, na ungekuwa huko nje gizani kwenye uwanja mkubwa. Nasi tunajua ya kwamba Franklin, na kadhalika, wamethibitisha hilo, sayansi, kwamba umeme uko hewani. Sasa, hebu chukua waya wa shaba, na uinue juu, kisha uuangushe chini, nawe... umeme tuli, umeme utaushika, mpaka

karibu utaiwasha dunia, kama ulikuwa maili moja juu hewani, ungeichoma dunia.

¹⁹ Sasa, ungeweza kusimama nje katika uwanja huo na kupiga mayowe kwa sauti kuu utakavyo, “Nimepotea, nimepotea! Ewe umeme mkuu, njoo sasa na uiangazie njia ya kupanda juu, nipate kuliondokea giza hili,” kamwe hautakuja. Lakini kama utafanya kazi kulingana na kanuni za umeme, mbona, utaiangazia hiyo njia ya kupandia, upate kuondoka uende. Lakini inakubidi kufanya kazi kulingana na kanuni hizo.

²⁰ Sasa, Mungu ana sheria, pia. Na kuna uponyaji na wokovu katika azimio la Mungu kwako, kama utafanya kazi kulingana na mipango Yake, na sheria Zake juu ya hayo. Kwa hiyo hivyo ndivyo tunavyopaswa kupanga mkutano, hivyo ndivyo. . . Mara saba kote ulimwenguni, nimekuwa kwenye jamii mbalimbali, namna za watu kwa makumi elfu, nimeona mambo makuu ambayo Bwana wetu amefanya, lakini daima ninaona ya kwamba inahitaji watu ambao watajinyenyekeza, na kuweka kando mawazo yao wenyewe kulihusu, na kuchukua tu wazo la Mungu juu yake, na kufanya kazi kulingana na mpango Wake, ambalo ni imani katika yale aliyosema.

²¹ Sasa, tunaamini ya kwamba Mungu ni Mwenyezi Mungu. Hapa katika chuo cha Kikristo, na kwenye uwanja huu, na pamoja na Wakristo, nina hakika sote tungeweza kusema kwa moyo mkunjufu, “Amina,” kwa hilo, kwamba Mungu ni Mungu, Yeye ni Mungu yeye yule, kama sivyo, kamwe hakuwa Mungu. Kama Yeye. . . Na Mungu huyo hana kikomo. Yeye hana kikomo, yuko kila mahali, anajua yote, yuna nguvu zote; Yeye ni Mungu. Kama sifa hizo haziko ndani Yake, Yeye si Mungu. Naye ndiye Yule mkuu wa Milele. Kamwe hukuanza, kamwe hatakoma.

²² Na ni ninii tu, chochote kilicho na mwanzo kina mwisho, ni yale tu ambayo hayakuanza, hayana mwisho, hayo ni ya Milele. Umilele hauna mwanzo wala mwisho. Na njia pekee tunayoweza kuwa na Uzima wa Milele ni kupokea sehemu Yake ndani yetu, na hilo linatufanya wana na binti wenye Uzima wa Mungu ndani yetu. Ndipo tunao Uzima wa Milele, kwa kuwa sisi ni wana na binti za Mungu, kwa hiyo sisi ni wa Milele pamoja na Mungu, tunapoupokea Uzima wa Milele. Kuna njia moja tu ya kufanya hivyo, hiyo ni kuzaliwa na Roho Mtakatifu. Njia pekee tunayoweza kuwa na Uzima wa Milele ni kuzaliwa kwa Roho Wake.

²³ Sasa, basi kama Mungu, akiwa hana kikomo, Naye ameninii. . .basi Yeye ni mkamilifu, Anaweza. . .na kama Mungu akiwahi kuitwa jukwaani kufanya uamuzi juu ya jambo fulani, kama jinsi anavyofanya uamuzi Wake wa kwanza, sasa msisahau hili, wakati ibada zikiendelea, jinsi anavyofanya uamuzi Wake wa kwanza, uamuzi Wake unaofuatia hauna budi kuwa ni kitu kile kile, na kila uamuzi atakaofanya baadaye

hauna budi kuwa vile vile. Kama akiubadilisha, basi Yeye alikosea alipofanya uamuzi Wake wa kwanza.

²⁴ Mnaona, sisi tuna kikomo, sisi, ninaweza kusema, jambo fulani, inanibidi kulighairi, kwa sababu mimi ni mwanadamu. Aliye mwerevu sana miongoni mwetu hana budi kulighairi mwaka baada ya mwaka.

²⁵ Miaka mia tatu iliyopita, mwanasayansi Mfaransa alithibitisha kwamba kwa kufingirisha mpira juu ya dunia, na akasema kama—kama ninii...m—mtu akiwahi, angeweza kupata nguvu za kutisha za mwendo wa maili thelathini kwa saa, nguvu za uvutano zilithibitisha ya kwamba yeye angeondoka duniani.

²⁶ Sasa, nawaambia, sayansi haitaangalia nyuma na kusema yale waliyosema, maana wanaenda yapata maili elfu mbili kwa saa sasa, na kwenye...wanakaa ardhini kwenye mwendo wa maili mia nne ama mia tano kwa saa. Mnaona? Kwa hiyo wasingangalia nyuma kwenye yale waliyosema. Lakini hata hivyo, lilikuwa ni thibitisho la kisayansi ya kwamba wao, kwa njia fulani, walifingirisha mpira, na kwa mwendo huo, walisema maili thelathini kwa saa ungemwondosha duniani. Sasa, ningeninii...Hilo ni dhahaka siku hizi. Kwa hiyo tunaona, ya kwamba katika jambo hili, hatuna budi...Hao jamaa walikuwa na kikomo, hivyo ndivyo vizuri sana walivyojua, nisingemhukumu mtu huyo kwa jambo hilo, hilo lilikuwa ndilo jambo zuri sana alilojua. Lakini mnaona, hana budi kubadilisha mawazo yao sasa, kwa sababu kwanza kabisa halikuwa sawa, bali hiyo haiwezi kuwa ni Mungu.

²⁷ Mungu akisema lolote, Yeye hana kikomo, na hilo ni “kamilifu.” Kama Mungu aliwahi kuitwa jukwaani kumwoko a mtu anayeililia nafsi yake iliyopotea, halafu Mungu akamwoko a kwa msingi wa kanuni fulani, azimio la kanuni, , basi kama kanuni zizo hizo zikitimizwa na mtu mwingine, basi kila mtu anayemwendea Mungu, Yeye hana budi kutumia mfumo uo huo. Naye itambidi kufanya hivyo, kama matakwa hayo yametimizwa, basi itambidi Mungu kutenda vivyo hivyo, asipofanya hivyo alikosea wakati alipomwoko a mtu wa kwanza.

²⁸ Na kama mtu huonywa juu ya msingi wa imani yake, mtu, mtu mgonjwa alimwita Mungu, na mgonjwa huyu, wakati akimwita Mungu, Mungu alimponya kwa sababu ya imani yake, kama mtu mwingine akimwita Mungu, akitumia imani iyo hiyo, Mungu hana budi kutenda vivyo hivyo. Mnaona? Kwa hiyo ninajaribu kuwafanya mwone.

²⁹ Kuna mengi sana nchini siku hizi ambayo yako chini ya kitengo cha uponyaji wa Kiungu ambayo hayapaswi kamwe kuwa hudumani. Ni namna fulani ya mhemuko, na—nawe unaweza kudanganywa na mihemuko, bali Neno Ndilo linalosimama, Neno la Mungu la Milele. Mungu si bora kuliko

Neno Lake, wala hakuna mtu aliye bora kuliko neno lao, kwa hiyo ni kurudi kwenye Neno.

³⁰ Sasa, simaanishi kusema ya kwamba Mungu hafanyi mambo ambayo hajayaandika katika Neno Lake. Angeweza kufanya chochote atakacho pia, huyo ni Mungu. Lakini kama nitaninii tu... Kuna mengi yaliyoandikwa *Hapa* kwa ajili yangu, kama tu ninaweza kufanya *hili* litimie, kwamba, ahadi alizotoa Yeye, basi ninajua, linaweza kuungwa mkono na Neno la Mungu, kwa hiyo ni Mungu, hivyo tu.

³¹ Sasa, tutakumbuka hilo tunapoendelea. Kumbukeni Mungu hana kikomo, hawezi kubadilika, Ni yeye yule jana, leo, na hata milele; hana budi kudumu na Neno Lake. Kama Mungu... Kama *Hili* si Neno la Mungu, basi kanisa Katoliki liko sahihi kabisa, ni kanisa badala ya Neno. Lakini kama *Hili* ni Neno, katika Kitabu cha Ufunuo, mlango wa 22, Mungu alisema, “Yeyote atakayeondoa Neno kutoka kwa *Hili*, ama kuongeza chochote Kwake, huyo ataondolewa sehemu yake katika Kitabu cha Uzima.” Kwa hiyo *Hili* ndilo Kweli.

³² Sasa, huenda nisiwe na imani ya kuyafanya yote kutimia, kama vile Henoko aliyemwamini Mungu sana, mpaka alipofanya matembezi ya alasiri pamoja Naye, halafu akachoshwa tu na kukaa duniani, na akapanda juu Nyumbani pamoja Naye, huenda nisiwe na imani ya namna hiyo, lakini kamwe sitamzuia mtu mwingine, ambaye ana imani ya namna hiyo, nita—nitamshukuru Mungu kwa ajili ya mtu anayeweza kufanya matembezi ya alasiri, na isimbidi kufa, kisha apande juu moja kwa moja pamoja Naye. La—laiti ningalikuwa na imani hiyo, natumaini kuwa nayo mwishoni mwa safari, ama, kabla ya wakati huo, nikiweza.

³³ Kwa hiyo kile tulicho nacho, tuko hapa kuvuta pamoja, si kitu kipya, bali ni Injili ile ile ambayo mmehubiriwa wakati wote, niko hapa tu kuweka wavu wangu pamoja na ndugu hawa hapa, na kuvuta pamoja, kama kundi la watu kwa ajili ya Ufalme wa Mungu, kulipa Kanisa maisha mapya, kuweka huduma yangu pamoja na huduma ya wanaume hawa. Hatujagawanyika, sisi ni ndugu. Wala hatuko hapa kuongeza kitu kwake, wala kuondoa kitu, tuko hapa kuyakuza yale ambayo tayari yamehubiriwa, na yale tunayoamini, kama watoto wa Mungu aliye hai.

³⁴ Yesu alisema, “Ufalme ni kama mtu aliyeenda baharini, akatupa jarife, alipolitoa, alikuwa na wa kila namna.” Hao ndio jarife la Injili hushika, hushika ninii, wa kila namna: kasa, vyura, nyoka, mijusi, na kadhalika. Jarife la Injili litafanya hivyo. Si kazi yangu kusema yupi ni yupi au mtu yeyote yule, Mungu ndiye anayeamua. Huyo ni Mungu.

³⁵ Lakini ninaninii tu... Mtu fulani anasimama pembeni, akivua samaki, akitupa wavu wake ndani na kuuvuta, mtu mwingine anapitia hapo na kumsaidia, hivyo ndivyo tu

nimefanya hapa Bloomington, ni kuja, kwa sababu nilijisikia kuongozwa na Roho Mtakatifu kuja, na kuweka wavu wangu pamoja na ndugu zangu, na kuutupa nje kote humu nchini, na kuvuta kwa ajili ya Ufalme wa Mungu, pamoja nao, kuwaingiza watu wote tuwezao.

³⁶ Sasa, uponyaji wa Kiungu ni jambo dogo. Kamwe huwezi kulifanya kubwa jambo dogo, mtu yeyote anajua hilo, mnaona, huwezi kufanya hivyo. Lakini hata hivyo, kama vile Dk. F. F. Bosworth, mmoja wa mameneja wangu, alikuwa katika huduma za ng'ambo pamoja nami, na hivi majuzi tu akaenda Nyumbani Utukufuni, umri wa miaka themanini na minne, alikuwa... alisema, "Ndugu Branham, uponyaji wa Kiungu ni kama chambo ulichoweka kwenye ndoana kumshika samaki. Kamwe humwonyeshi samaki ndoana, unamwonyesha chambo, yeye huuma chambo akashikwa na ndoana." Kwa hiyo hivyo ndivyo ifanyavyo.

³⁷ Uponyaji wa Kiungu na nguvu za Mungu za kuwaponya wagonjwa, huvutia usikivu wa watu, na unapofanya hivyo, basi unaweza kuiacha Injili iende ikawakamate kwenye jarife na kuiponya nafsi, ambayo ni mara mamilioni zaidi ya uponyaji wa mwili. Hiyo ni kweli. Bwana awabariki ndilo ombi langu.

³⁸ Sasa, *Hili* ni Neno la Kiungu, nami ninaliamini kwa uchaji tangu jalada hadi jalada. Nami naituliza nafsi yangu juu ya fungu lolote la maskini Biblia hii iliyobarikiwa. Nimekuwa nikilihubiri sasa kwa miaka thelathini na mmoja, kote, kote ulimwenguni, wala sijapata kuliona likishindwa bado. Nami... Halitashindwa. Mradi ni Mungu, nasi tuna imani ya kuunga mkono yale aliyosema, basi Mungu atafanya yale aliyosema angefanya.

³⁹ Yesu alisema ya kwamba Neno la Mungu ni kama Mbegu ambayo mpanzi alipanda. Na mbegu yoyote itakayoanguka kwenye ardhi nzuri, yenye rutuba itazaa kwa aina yake. Na kama, ninaweza tu, kwa msaada wa Roho Mtakatifu, kuitupa hiyo Mbegu moyoni mwako, ndani ya moyo wa asiyeamini, ndani ya moyo wa mtu vuguvugu, ndani ya moyo wa mgonjwa, acha Mbegu hiyo ipate Uhai, kama iko katika ardhi nzuri na katika hali nzuri, itaishi.

⁴⁰ Hivi majuzi niliona mahali waliposhuka kwenda Misri, wana alizeti, mbegu iliyokuwa mle ndani karibu, nasahau ilikuwa miaka elfu ngapi, baadhi ya ngano iliyokuwa ghalani, Yusufu aliweka mle huko nyuma kabisa miaka elfu mbili mia tano iliyopita ama zaidi, akaipanda ardhini nayo ikazaa zao la ngano, maana ilikuwa imerutubishwa, chembechembe hiyo inakaa mle ndani.

⁴¹ Na watu wowote watakaochukua Mbegu ya Mungu moyoni mwao, chini ya hali ifaayo itatoa kile hasa inachosema. Nimeona

kansa ya sarkoma ikiponywa Nayo, nami ninajua ya kwamba ni kweli.

⁴² Sasa, kwanza, haina budi kuja katika udongo mzuri, na udongo huo sio theolojia, udongo huo ni imani. Laiti tungaliweka kando theolojia yetu kwa muda kidogo, maana tunatofautiana, na hebu tuwazie tu juu ya imani tutakayozungumzia.

⁴³ Sasa, hivi uliwahi kupanda...kumwaga njia ya mguu wakati wa kipupwe? Zao lako kubwa zaidi la nyasi liko wapi? Pembeni, kwenye kingo za hiyo njia. Mbona hivi? Mbegu hiyo iliyoanguka kutoka kwenye nyasi hiyo chini ya njia hiyo, imefunikwa na zege, lakini j-u-a ndilo mtoa uhai wa uhai wote wa mimea, haina budi kuja wakati jua liko katika hali fulani, majira ya kuchipua yenye joto sana la jua yatautoa uhai huo. Wala huwezi kuuficha, nyasi hiyo inaweza kuzikwa katikati ya njia hiyo ya miguu, bali acha jua lenye joto liwe sawa kabisa, utafanya...huwezi kuuficha uhai huo, utapenya moja kwa moja na kuchomoa kichwa chake moja kwa moja kwa sifa za Mungu, na, kwa sababu jua, j-u-a, linawaka.

⁴⁴ Siku moja, M-w-a-n-a atakuja, Mwana wa Mungu, uhai wote, haidhuru uko wapi, huo ni uhai uliozaliwa mara ya pili, uliuorutubishwa kwa Neno la Mungu, utatokeza, sijali kama umezikwa kwenye majivu, chini ya bahari, utafufuka katika mfano wa Muumba, na utaishi milele, hilo ni Neno la Mungu. Na tuinamishe vichwa vyetu sasa, tunapozungumza na Mwandishi Wake, kwa dakika chache.

⁴⁵ Mungu mwingi wa Neema na Mtakatifu, Yule aliyemfufua tena Yesu katika wafu, tunakushukuru kutoka kwenye kilindi cha moyo wetu kwa ajili ya tendo hili kuu, na hakikisho hili kuu ya kwamba alijeruhiwa kwa makosa yetu, na akachubuliwa kwa maovu yetu, adhabu ya amani yetu ilikuwa juu Yake, na kwa kupigwa Kwake sisi tuliponywa, na kwamba tunajua ya kwamba tumetakaswa kwa kuoshwa kwa maji kwa Neno, sasa tunao Uzima wa Milele kwa neema ya Mungu, Hazina hii tunayoshikilia katika vyombo hivi vya udongo, visivyowekwa mle ndani na mwanadamu, bali kwa nguvu za ufufuo wa Mungu.

Nasi tunamsikia mshairi wakati alipoandika:

Alipoishi, alinipenda; akifa, Yeye aliniokoa;
Alipozikwa, alizipeleka dhambi zangu mbali sana;
Alipofufuka, alinihesabia haki bure milele:
Siku moja, Yeye yuaja—loo, siku yenye utukufu!

⁴⁶ Tunangojea na kuugua pamoja na maumbile, Bwana, twaitamani ile Siku kuu ambayo inakuja hivi karibuni. Nasi tunaomba, Baba, ya kwamba utaichunguza mioyo yetu usiku wa leo, na kukiwako na dhambi yoyote, ambayo ni

kutokuamini (Haidhuru sisi ni wa kidini jinsi gani, kama tungali hatuliamini Neno la Mungu, sisi ni wenye dhambi, “Kwa maana asiyeamini amekwisha kuhukumiwa.” Kwa maana tunajua Siku ile siri za mioyo yote zitafichuliwa.), Nuru ile kuu ya Mungu inayochunguza itaichunguza mioyo yetu usiku wa leo na kuona kama kuna kitu chochote kichafu kwetu, kutokuamini kokote katika Mungu ama Neno Lake, basi utusafishe, Bwana, na hayo yote, ili kwamba kwa mara mara nyingine tena, hapa Illinois, tuone uamsho mkuu unaoenea.

⁴⁷ Bwana, tunaomba ya kwamba utaanzia papa hapa Bloomington, uenee jimboni kote na nchini kote. Jalia hapa miongoni mwa watu hawa waliokusanyika usiku wa leo, katika makanisa haya yote yanayoshirikiana, kwamba nguvu za Mungu zitadhihirishwa sana miongoni mwao, hata wataona na kujipa moyo mpya tena.

⁴⁸ Kijalie chuo hiki, Bwana, ambacho kimeturuhusu kuwa na jumba hili la mikutano, kutakuwa na uamsho utakaotokea hapa, kama huko Wheaton, na huko chini Asbury, na sehemu zingine nyingi, utakuwa ni mkutano wa maombi ya mchana na usiku, Bwana, hata watu watakuja kutoka mashariki hadi magharibi. Mungu, wape uamsho wa mtindo wa kale, wa John Wesley, bidii inayowaka ya mioyo ya hawa vijana, ambao wangeondoka chuoni hapa, wapate kwenda kama Asbury mwingine, na utujalie, Baba. Tupe neema Yako. Tunayaweka maisha yetu wakfu Kwako, na ibada Kwako, na yote tuliyo nayo, kiakili na kimwili pia. Nena nasi, Baba, tunaomba, katika Jina la Yesu. Amina.

⁴⁹ Katika Neno usiku wa leo, ambalo ninaamini ya kwamba hakuna mkutano . . . Huu ni maskini usiku tu wa kuja pamoja, ili kwa namna fulani tupate kufahamiana. Ninatambua ya kwamba mimi ni mgeni kwa wengi wenu, bali nisingewataka mjisikie hivyo, kwamba . . . Mimi ni ndugu yenu, nami nipo hapa kwa ajili ya kuwasaidia, nanyi kunisaidia kumjua Kristo vizuri zaidi.

⁵⁰ Basi tufungue somo linalojulikana, na wale ambao wamefuatilia huu uamsho, niliwazia, ninii tu, ningezungumza kwa dakika hizi chache juu ya somo hili, ambalo huenda likatoa msingi wa mwanzoni wa kile tunachojaribu kuwaelezea watu. Yohana Mtakatifu 12:20, na katika Waebrania 13:8, na, pia, huenda tukarejea kwenye Kitabu cha Matendo ninii wa 3 . . . , ama, kifungu cha 3, 1:3.

Palikuwa na Wayunani kadha wa kadha miongoni mwa watu waliokwea kwenda kuabudu kwenye sikukuu:

Basi hao walimwendea Filipino, mtu wa Bethsaida ya Galilaya, wakamwomba, wakisema, Mabwana, sisi tunataka kumwona Yesu.

⁵¹ Na katika Waebrania 13:8, inasema:

Yesu Kristo ni yeye yule jana, . . . leo, na hata milele.

52 Matendo 3, ama, 1:3:

Yesu aliwadhahirishia nafsi yake kwa dalili nyingi zisizoweza kukosea, . . . (Ishara nyingi zisizoweza kukosea ambazo aliwaonyesha watu kwamba amefufuka katika wafu.)

53 Sasa, tungetaka kuwaulizeni swali hili, usiku wa leo, nami nawatakeni msikilize kwa makini sana kwa sababu mikutano ya siku za usoni itategemea kitu cha namna hii. Hivi nimesoma kutoka kwenye Neno la Mungu, ama Hicho ni kitabu kingine tu? Ni Neno la Mungu, basi ninaliamini kwa moyo wangu wote.

54 Sasa, kama ni Neno la Mungu, kuna swali lililoulizwa hapa, nalo liliulizwa na Myunani, ama Wayunani, hasa, huenda nikasema. Walikuja kwenye karamu ya Sikukuu ya Pentekoste, nao walitaka kumwona Yesu, nao wakamwendea Filipo, aliyekuwa ni mtu wa Bethsaida ya Galilaya, wakasema maneno haya: “Mabwana, sisi tunataka kumwona Yesu.” Nasi tunatambua ya kwamba Filipo, yule mtumishi wa Kristo, alilishughulikia hata wakatimiziwa haja yao. Walimwona, kwa sababu walikuwa ni watu wenye mioyo yenye njaa, iliyotamani kumwona Yesu.

55 Nami siamini ya kwamba kuna mtu yeyote ambaye amewahi, wakati wowote, amewahi kusikia ama kusoma habari za Yesu, ila ambaye angetamani kumwona. Nina hakika hiyo ingekuwa ndiyo shauku ya kila moyo wa Ukristo, kumwona Bwana Yesu. Hiyo ndiyo sababu tunafanya kazi, na ndiyo sababu tunaweka kando kila kitu kujaribu kuishi ili kwamba tuweze kumwona Yeye siku moja. Lakini sijui, kama Maandiko yanasema dhahiri ya kwamba ni yeye yule jana, leo, na hata milele, basi kwa nini hatuwezi kumwona siku hizi?

56 Sasa, tuna haki ya kuomba kumwona kama wale Wayunani walivyooomba kumwona. Walisema, “Mabwana, sisi tunataka kumwona Yesu.” Na kwa kumwomba mtumishi wa Kristo, mtumishi huyu aliweza kumtoa Yesu wapate kumwona. Kamwe hawakuomba kuziona kazi Zake, ama kusikia hekima Yake, waliomba tu kumwona Yesu. Nao walipewa majaliwa hayo na mtumishi wa Kristo.

57 Sasa, tumepita siku chache tu tangu tuusherehekee ufufuo. Na kwa wengi wa wale tunaowaita siku hizi, Wakristo, huo ndio umbali unaopata kwenda, ni kwenye Pasaka kutambua ya kwamba hiyo ni siku ya ukumbusho wa tukio la kihistoria, bali ni zaidi ya hayo. Hiyo ilikuwa tu siku uliyoanza, sasa unaendelea mbele zaidi na zaidi, hauna mwisho, Yeye yu hai milele.

58 Na kama vile Luka, akiandika Matendo ya mitume, ama, matendo ya Roho Mtakatifu ndani ya mitume, miaka sitini na mitano baada ya tukio hilo, alisema ya kwamba alijionyesha Mwenyewe kwa dalili zisizoweza kukosea, kwa ishara, ishara

zisizoweza kukosea, kwamba Yeye alikuwa ni Yesu yeye yule aliyekuwa ametembea duniani, alijionyesha Mwenyewe yu hai kwa ishara zisizoweza kukosea, ya kwamba alikuwa ni Bwana Yesu aliye hai, aliyefufuka.

⁵⁹ Sasa, miaka elfu moja mia tisa imepita tangu wakati huo, ama zaidi, lakini hilo halimaanishi hata nukta moja ndogo kwa Umilele. Kama tungalikuwa hapa miaka milioni kumi bado isingekuwa...kama tu ilivyokuwa, kama ule msemu wa kale ulivyo, “Huyo mtu alikuwa wapi wakati aliporuka kutoka kwenye daraja?” Mnaona, usingeweza kulielewa. Mtu fulani alisema, “Ndani ya maji.” Hakuwa ameruka bado. Kasema, “Juu ya daraja.” Vema, ye—ye—yeye angali juu ya daraja, hajaruka. Kwa hiyo yeye...Mnaona, huwezi...Hakuna mwanzo wala mwisho wake.

⁶⁰ Sasa, vivyo hivyo kwa Kristo, kama amefufuka katika wafu, Kristo asiyeweza kukosea, basi Yeye ni yule yule leo alivyowahi kuwa, la sivyo Maandiko yanapatikana na makosa.

⁶¹ Sasa, basi nashangaa usiku wa leo, ni wangapi katika kusanyiko hili linaloonekana wangetaka kuinua mikono yao na kusema, “Ningependa kumwona Yesu. Mabwana, sisi tunataka kumwona Yesu”?

⁶² Vema sasa, hebu tuone, kama *Hili* ni Neno la Mungu, tunaliadini. Sasa, kama tungetamani kumwona Yesu, yapata Wayunani wawili tu ndio waliokuja na kutaka kumwona na shauku yao ikatimizwa, kwa hiyo kuna angalau mia mbili, ama tatu, hapa ndani usiku wa leo, na wengine wengi wako hapa wakitaka kumwona Yesu, kwa hiyo kama alikuwa tayari kujionyesha Mwenyewe kwa hao Wayunani wasiotahiriwa, kwa sababu walitaka kumwona, ni zaidi sana jinsi gani anavyopaswa kujionyesha Mwenyewe kwa watoto Wake ambao wameokolewa na kuzaliwa kwa Roho wa Mungu aliye hai? Kwa nini asiwe tayari zaidi kujionyesha Mwenyewe hai kwetu usiku wa leo, kama alivyokuwa kwa wale arobaini, na wengine mbalimbali, kama alivyokutana nao katika jamii? Ni swali, bali ni ahadi.

⁶³ Na basi kama Waebrania 13:8 ilisema ni yeye yule jana, leo, na hata milele, basi hana budi kuwa yeye yule katika kanuni, yeye yule katika nguvu, yeye yule kwa kila njia aliyokuwa jana, la sivyo Yeye si yeye yule.

Mtu fulani anasema, “Ni yeye yule kwa njia fulani.”

La, Yeye ni yule yule, Maandiko yanasema. Huyo ni Yesu yule yule aliyekuwako, aliyeko leo, na atakuwako milele.

⁶⁴ Sasa, kama ningepitia kwenye kusanyiko hili la watu, na kusema, “Wabatisti, Wamethodisti, Wapentekoste, wa—wa aina mbalimbali, mnafundisha hayo kanisani mwenu?”

“Naam, hakika, tunafundisha.”

⁶⁵ Vema, hivyo ndivyo unavyopaswa kufanya, hiyo ni kweli, kwa sababu ni Neno la Mungu lisilokosea. Lakini hivi uliwahi kujaribu kumwomba Mungu alidhihirishe, kulifanya halisi kwako, sio tu kama Kristo wa kihistoria, bali Kristo aliyefufuka?

⁶⁶ Sasa, watu wengi wanamkubali Kristo kama—kama Mwokozi wao, kwa sababu wanaogopa kuzimu, wengine wana—wanaogopa kufa bila Yeye, lakini umemkubali Yeye kama Bwana wako, Yeye awezaye kusimama katika sehemu yako ya ndani kabisa, na kuifungua milango ya imani yako, na—na ujiachilie tu uwe mikononi Mwake? Nina hakika kama ukifanya hivyo, Yeye ataitikia kila ahadi *Hapa* ndani kwa, “Amina,” kwa kuwa Roho Wake Mwenyewe aliyelandika Biblia, yuko hapa kuifanya iseme, “Amina,” kwa sababu Yeye ndiye Mwandishi wa Biblia hii. Halafu basi, kama tu utamwamini na kuufungua moyo wako, basi tutamwomba sasa, kama atakuja na kujitambulisha Mwenyewe kwetu, kama alivyofanya.

Vema sasa, huenda nikasema, “Mngeweza...? Mnampata katika kanuni zenu za imani za Kibaptisti?”

“Naam.”

“Kanuni za imani za Kimethodisti?”

“Naam.”

“Kanuni za imani za Kipentekoste?”

“Naam.”

⁶⁷ Hiyo ni kweli, chunguzeni kama huenda imeandikwa mle ndani. Lakini hebu na tuulize jambo hili, kama lilivyosema ya kwamba Yeye ni yeye yule leo kama alivyokuwa jana, basi hebu...

⁶⁸ Kama ningeiendea kanuni yenu ya imani ya Baptisti, ama kanuni ya imani ya Methodist, ama kanuni ya imani ya Pentekoste kuomba kitu kama hicho, mngesema, “Vema, ni *hivi-na-hivi*.” Na mmoja angesema, “La, iko *hivi*.” Na mwingine angesema, “La, kanuni yetu ya imani inasema *hivi*. Tumefundishwa *hivi*.” Kungekuwa na mawazo tofauti juu yake. Lakini njia pekee ya kulifanya hivyo kwa haki, ni kurudi nyuma na kuona kile alichokuwa jana, na yale aliyofanya jana, jinsi alivyotenda jana, kisha tuone kama atakuja na kuwa kitu kile kile leo.

⁶⁹ Sasa, kila mtu anaamini na anajua ya kwamba mwili wa nyama wa Bwana Yesu umeketi mkono wa kuume wa Mungu Mwenyezi, kwenye Kiti cha Enzi cha Mungu, akituombea tunapokiri. Nyote mnaamini hilo? Naye Roho Mtakatifu yuko hapa, ambaye alikuwa juu Yake, ambaye alikuwa ni Mungu katika Kristo, sasa huyu ni Mungu katika Kanisa Lake. Mungu alikuwa katika Nguzo ya Moto wakati mmoja, yule Logos aliyetoka kwa Mungu, huyo alikuwa ni yule Malaika wa agano aliyeeenda pamoja na wana wa Israeli nyikani, ndipo

akadhihirishwa, Mungu yeye yule katika mwili, ambaye alikuwa ni Mwanawe, ambaye alimtia uvuli bikira, akaumba Seli ya Damu, na kuishi katika mwili huo wa nyama, Mwana wa Mungu.

⁷⁰ Sasa, basi wakati Mwana huyo wa Mungu, alipoutoa uhai Wake na mwili Wake kwa ajili ya dhabihu, Kisha Mungu akaufufua mwili Wake katika siku ya tatu, na kumweka kwenye mkono Wake wa kuume huko Juu, ndipo Roho Mtakatifu alirudi, na kwenye Siku ya Pentekoste, Biblia ilisema, “Kulikuwa na Ndimi za Moto,” kama ndimi, kama mwali wa moto, “ukamkalia kila mmoja wao,” huyo alikuwa ni Mungu, Roho Mtakatifu yeye yule aliyekuwa nyikani pamoja na wana wa Israeli.

Unasema, “Kwani huyo hakuwa ni Yesu?”

⁷¹ Alikuwa. Baada ya kifo Chake, kuzikwa, na kufufuka, Sauli alikuwa akienda zake Dameski, ndipo Nuru kuu ikamwangusha chini. Yesu akiwa duniani, alisema, “Nalitoka kwa Mungu, na ninaenda kwa Mungu.” Na baada ya kifo Chake, kuzikwa, na kufufuka, na kupaa Kwake, Sauli, akienda zake Dameski, alibwagwa chini. Ndipo akaangalia juu na kulikuwa na Nuru iliyompofusha, ndipo akapaza sauti, “Sauli, Sauli, mbona unaniudhi?”

Akasema, “U nani Wewe, Bwana?”

Akasema, “Mimi ni Yesu,” alikuwa amerudi kwenye Nguzo ile ile ya Moto iliyowaongoza wana wa Israeli nyikani.

⁷² Yohana Mtakatifu mlango wa 6, walikuwa wakijadiliana Naye juu ya mawazo mbalimbali na kadhalika, na kusema, “Ulisema wewe u rika moja na Ibrahimu,” kisha kasema, “ulisema umemwona Ibrahimu, nawe ni mtu asiyezidi umri wa miaka hamsini, sasa tunajua una wazimu na una pepo.”

⁷³ Akasema, “Ibrahimu asijakuwako, MIMI NIKO.” Kabla hakujakuwako, Yeye alikuwako, kwa sababu alikuwa ndiye *MIMI NIKO* aliyekuwa katika kile kijiti kilichowaka moto. Ile Nguzo ya Moto iliyowaongoza wana wa Israeli nyikani ilikuwa ni Mungu yeye yule aliyedhihirishwa katika Yesu Kristo, akafa, akapaa Juu, na kumrudisha Roho Mtakatifu. Na katika Yohana 14—Yohana 14:7, ilisema, “Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi, yeye naye atazifanya, kubwa kuliko hizi atafanya, kwa kuwa mimi naenda kwa Baba Yangu.”

⁷⁴ Yohana Mtakatifu m—mlango wa 5 na kifungu cha 19 cha mlango wa 5, Yeye alisema, “Amin, amin, nawaambia, Mwana hawezi kutenda neno Mwenyewe, bali lile amwonalo Baba analitenda, ndilo atendalo Mwana vile vile.” Alifanya kama Mungu alivyomwonyesha, kwa hiyo akasema, “Nawaambia, siwezi kutenda neno.” Yeye hakudai kuwa Mponyaji wa Kiungu, alisema alifanya tu kama alivyoona kwa ono yale Mungu aliyomwambia afanye, na akaahidi Kanisa litafanya vivyo hivyo.

⁷⁵ “Bado kitambo kidogo na ulimwengu hautaniona tena, bali ninyi mtaniona,” sasa angalieni, *ulimwengu*, “kosmos,” ambalo linamaanisha *utaratibu wa ulimwengu*, “hautaniona tena,” wasioamini, “hawataniona tena, hata hivyo, ninyi mtaniona,” *ninyi*, waaminio, “kwa kuwa Mimi,” *mimi* ni kiwakilishi nafsi, “nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari.” Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele.

⁷⁶ Sasa, kama Yeye ni yeye yule, basi nguvu Zake, Uzima Wake uliofufuka unapaswa kuwa unaishi Kanisani, akileta huduma ile ile aliyokuwa nayo hapa duniani, kwa kuwa Yeye aliahidi. Sasa, wote hawawezi kuipokea hiyo, tunatambua hilo, watu wanazaliwa kwa ajili ya hukumu, Maandiko yanasema hivyo, lakini, “Yeye aliye na sikio, na alisikie Neno hili ambalo Roho aliambia Kanisa.” Mnaona?

⁷⁷ Sasa, hebu tuone kile alichofanya, na ndipo tutaona kile atakachofanya sasa; tuone kile alichokuwa, tuone kile alichochokuwa, na tuone kama tunaweza kumgundua Yesu Kristo katika kufufuka Kwake.

⁷⁸ Sasa, tunaona ya kwamba wakati alipochukuliwa mimba na bikira na kuzaliwa, ki—kisha kwenye umri wa miaka thelathini akabatizwa na Yohana Mbatizaji kwenye mto Yordani, na mara akaongozwa mpaka nyikani akajaribiwe na ibilisi, naye akakaa huko siku arobaini, ndipo akatoka na kuanza huduma Yake ya duniani.

⁷⁹ Hebu na turudi kwenye mlango wa kwanza wa Yohana Mtakatifu sasa, kwa kuwa, tumeanza kwenye Kitabu cha Yohana Mtakatifu. Na wakati juma likiendelea, tutaendelea kuchukua hili na kulifunganisha kutoka Mwanzo hadi Ufunuo hivi kwamba hakuna mkosoaji mwenye akili timamu, ama hakuna njia hata kidogo, anayoweza kulipinga. Ni Mungu.

⁸⁰ Mungu yuko katika Neno Lake. Mnaamini hilo? “Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwa pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno alifanyika mwili, akakaa miongoni mwetu,” Yohana Mtakatifu 1. Na katika Waebrania mlango wa 4, ilisema ya kwamba, “Neno la Mungu ni kali kuliko upanga ukatao kuwili, likichoma hata kugawanya mfupa, naam, Mtambuzi wa mawazo ya moyo,” Neno, wakati linapofanyika mwili ndani yetu.

⁸¹ Sasa, tunaona Yesu, mara baada ya Yeye kuanza huduma Yake ya duniani, alianza kuwaponya wagonjwa. Sasa, sikilizeni kwa makini, watu hao walikuwa wakimtazamia Masihi, Wayahudi walikuwa wakimtazamia.

⁸² Kuna matabaka matatu tu, ama, jamii tatu za watu duniani, hizo ni watu wa Hamu, Shemu, na Yafethi, wale wana watatu wa Nuhu, kama tunaamini Ne—Neno la Mungu. Ambapo wote walitokea humo, kwa sababu yale maangamizi yaliyotangulia gharika yaliwaangamiza wote mbali na hao, ulimwengu wote

uliangamizwa. Na kutoka kwa hao wavulana watatu zikatokea, jamii zote za dunia, na hao kama mkiangalia, hao walikuwa ni Myahudi, Mmataifa, na Msamaria.

⁸³ Petro alipewa, katika Mathayo Mtakatifu mlango wa 15, funguo za Ufalme. Kwenye Siku ya Pentekoste, aliwafungulia Wayahudi. Filipo akashuka na kuwahubiria Wasamaria na kuwabatiza, hata hivyo Roho Mtakatifu hakuwa amewashukia, ndipo akashuka na kuweka mikono juu yao nao wakampokea Roho Mtakatifu. Katika Matendo mlango wa 10, kifungu cha 49, kwamba Kornelio alikuwa ameona ono nyumbani mwake, akiwa Mmataifa, ndipo Petro akaona ono juu ya paa la nyumba aende huko, “Basi alipokuwa akisema maneno haya, Roho Mtakatifu akawashukia Mataifa.” Tangu hapo na kuendelea, kuna, ni wazi kwa ulimwengu wote basi: Myahudi, Mataifa, na Msamaria.

⁸⁴ Petro alikuwa na funguo, hizo zilikuwa ni yale mahubiri mazuri aliyohubiri, na kila kanisa, sijali kama ni Katoliki, Protestanti, popote, kama utakuwa Mkristo, inakubidi kurudi, na kanisa la kwanza ambalo Mungu aliwahi kuagiza lilikuwa kwenye Siku ya Pentekoste, lilikuwa ni kanisa la Kipentekoste linaloamini, lenye ujuzi wa Kipentekoste.

⁸⁵ Sasa, chukua *Baraza la Nikea*, ama *Wanzilishi wa Kanisa la Mwanzoni*, ama historia yoyote unayotaka, itakurejesha moja kwa moja, kanisa la kwanza lilikuwa ni kanisa la Kipentekoste, lililojazwa na Roho Mtakatifu, ishara, na maajabu, na miujiza ikifuata. Na kama Mungu ni Mungu asiye na kikomo na aliliweka Kanisa Lake katika utaratibu namna hiyo kwenye Siku ya Pentekoste, kila wakati atakapoliweka kanisa katika utaratibu, itakuwa ni jambo lile lile, halina budi kuwa, maana Yeye hana kikomo wala hawezi kubadilika. Mafundisho yetu na theolojia yametupeleka upande mmoja mpaka tunatangatanga nyikani, Biblia ya Mungu inabaki vile vile, na Roho wa Mungu anabaki vile vile. Hizi ni siku za mwisho, ni kurudi mahali ambapo nabii alisema itakuwa Nuru wakati wa jioni.

⁸⁶ Sasa, kama walikuwa wakimtazamia Masihi, ni wangapi wanaojua ya kwamba Wayahudi wanatafuta ishara, Wayunani hekima? Paulo alisema, “Sisi tunamhubiri Kristo aliyesulubiwa.” Sasa, Wayahudi, kumpokea Masihi, ilimbidi awe na ishara ya Masihi, kwa sababu Kumbukumbu la Torati mlango wa 18, kutoka kifungu cha 15 hadi cha 22, inathibitisha kile Masihi angekuwa. Na kama kile alichowaonyesha kama ishara Yeye alikuwa ni Masihi, hicho kitabaki katika vizazi vyote vijavyo, mradi kuna mtu wa kukipokea. Musa alisema katika Kumbukumbu la Torati mlango wa 18, kuanzia kifungu cha 15, “Bwana Mungu wenu atawaondokeshea Nabii miongoni mwenu, kama nilivyo mimi.”

⁸⁷ Naye huyo Masihi ilibidi awe Nabii, Mungu-Nabii, Naye angefanya ishara ya nabii. Pia katika sehemu zingine nyingi

katika Maandiko ambazo mimi...tungeweza kurejea, Mungu alisema, “Akiwepo mmoja miongoni mweni aliye wa kiroho, ama nabii, Mimi Bwana Mungu nitajitambulisha Mwenyewe kwake. Na yale nabii huyu asemayo, yaangalieni, yakitimia, basi msikieni, lakini yasipotimia, basi msimsikie.”

⁸⁸ Sasa, hiyo ilikuwa ndiyo ishara ya Israeli ya Masihi huyu mkuu, atakayekuja. Alikuwa awe Mungu-Nabii, aonyeshe ishara za nabii, kwa sababu nabii ndiye anayejiliwa na Neno la Bwana. Kwa hiyo katika kuja Kwake, kulikuwa kubadilishe kipindi chote cha wakati na kila kitu, na ingembidi kuwa na ishara ya nabii kuthibitisha ya kwamba Yeye alikuwa ni Nabii, ilimbidi kufanya hivyo, kwa sababu kila kitu kilikuwa kikibadilika, na hiyo ndiyo sababu ingewabidi kujua jambo hilo.

⁸⁹ Sasa, tunajua, kama Wakristo, ya kwamba Yesu alikuja jinsi hasa alivyotabiriwa kuja, lakini makanisa siku hizo yalikuwa yamegeuzwa vinginevyo. Walifikiri kwamba labda Mungu angeshusha ushoroba wa Mbinguni, Naye angeshuka juu ya mbawa za Moto ama chochote kile.

⁹⁰ Naye Yohana Mbatizaji, yule Eliya aliyekuwa anakuja, kwamba angekuwa jamaa fulani mashuhuri, kwa sababu milima ilikuwa iruke kama kondoo dume, nayo majani yalikuwa yapige makofi yao, na mahali palipoinuka pashushwe, na mahali paliposhuka, painuliwe. Vema, walitarajia jambo fulani kuu, la ajabu sana kulitikisa taifa, lakini alipokuja, yeye alikuwa ni nani? Alikuwa ni mtu aliyejizungushia kipande cha ngozi ya kondoo, amejaa ndevu usoni mwake, aliishi kwa nzige na asali mwitu, naye akaja akihubiri kwenye kingo za Yordani zenye matope, na kuyatikisa makanisa yapate kutubu.

⁹¹ Alipoona wengi wakija kwenye ubatizo wake, alisema, “Enyi wazao wa nyoka, ni nani aliyewaonya kuikimbia hasira? Msifikirie kusema moyoni mwenu, ‘Tunaye Ibrahimu baba yetu,’ kwa maana nawaambia ya kwamba Mungu anaweza katika mawe haya kumwinulia Ibrahimu watoto. Pia, shoka limewekwa penye shina la mti, kila mti usiozaa matunda mazuri hukatwa na kutupwa motoni.” Kwa hiyo mnaona, ilikuwa tofauti kabisa, wasingeweza kumpokea.

⁹² Wakati Yesu alipokuja, Yeye alikuja na jina haramu, alikuja kama mtoto aliyezaliwa nje ya ndoa takatifu. Kamwe hakwenda kwenye shule yoyote ya seminari, wala chochote kile tulicho na kumbukumbu yake katika Biblia, ama historia, kwamba aliwahi kuhudhuria shule siku moja, lakini aliwashangaza sana makuhani, kwa sababu alitumwa na Mungu, alikuwa na hekima na nguvu za Mungu kuunga mkono Kila kitu alichosema. Naye akawashangaza kwa Mafundisho Yake, kwa kuwa hakufundisha kama mwandishi, alifundisha kama mtu aliyekuwa na Neno la Bwana. Tumeona mafundisho Yake yalikuwa tofauti kabisa na

yale makanisa ya siku Zake yalikuwa nayo. Labda, ingekuwa ni tofauti sana siku hizi kama Yeye angalikuwa hapa.

⁹³ Sasa, tutaona, jambo la kwanza tutachukua katika Yohana Mtakatifu 1, tunaona ya kwamba kulikuwa na mtu jina lake Simoni, naye alikuwa na ndugu jina lake Andrea, walikuwa wavuvi. Sasa, sikilizeni kwa makini, msilikose hili. Kwa hiyo Andrea, labda, alizungumza na Simoni baada ya kushuka kwenda mkutanoni, na kumwona Roho Mtakatifu akishuka kama hua juu ya Bwana Yesu, Nuru hii kuu, ikishuka kutoka Mbinguni, kama, ilikuwa na mabawa, na kuangazia juu Yake, na Sauti ikisema, “Huyu ni Mwanangu mpendwa, ninayependezwa kukaa ndani Yake.”

⁹⁴ Ndipo basi tunaona ya kwamba hapana shaka alimwambia ndugu yake, kwa hiyo Simoni akaja njiani mwake kwenda kumwona Yesu. Farisayo aliyefunzwa vizuri, alijua baba yake alikuwa ni mwabudu mashuhuri wa Mungu naye alikuwa amefundisha jinsi ambavyo, jinsi Masihi atakavyokuwa wakati atakapokuja, akasema, “Kutakuwa na machafuko katika siku hiyo. Hapana shaka kwamba kutainuka mambo ya kila namna kukutangulia, ama, katika siku hiyo, lakini, Simoni, usisahau, Masihi huyu atakuwa ni Nabii wa Mungu, Naye ataonyesha ishara ya nabii, maana Musa alisema Bwana Mungu wetu atawaondokeshea Nabii. Kwa hiyo, kumbukeni, Yeye atakuwa ni Nabii, Simoni.” Sasa tunamtazamia Yeye jana.

⁹⁵ Ndipo Simoni akaenda kwa moyo mnyofu mbele za Mungu, akaingia mstarini ambapo Yesu alikuwa amesimama, mara Yesu alipomwona, na kumtupia macho Yake, Yeye alisema, “Jina lako ni Simoni, wewe ni mwana wa Yona.” Loo, ninawazia hilo liliondoa ugumu wote kutoka kwa Simoni! “Jina lako ni Simoni, nawe ni mwana wa Yona.”

⁹⁶ Labda Simoni alisitasita, na kumwangalia. Si kwamba tu alimjua, bali alimjua maskini baba yake mtauwa. Basi hapana shaka lilingia niani mwa Simoni, “Huyo Ndiye!” Basi akianguka miguuni pa Bwana Yesu, Yesu alisema, “Tangu sasa utaitwa Petro,” ambalo linamaanisha “jiwe dogo.” Naye akampa funguo za Ufalme.

⁹⁷ Kulikuwako na mtu aliyesimama pale jina lake Nathanaeli, aliona hili likitendeka, naye akajua bila shaka, ama, ninamaanisha Filipu, yule tunayenena habari zake usiku wa leo, aliona hilo likifanywa, naye akakimbia kuuzunguka huo mlima. Kama mtu yeyote hapa amewahi kuwa Palestina, kuangalia mahali walipotia alama, ni yapata maili kumi na tano kutoka mahali Yesu alipokuwa akihubiri, karibu na mahali alipompata rafiki yake, Nathanaeli. Akaenda na kubisha mlango, hapana shaka, akauliza Nathanaeli yuko wapi, mwanafunzi mashuhuri wa Biblia. Basi mke wake hapana shaka alisema, “Yuko huko

nyuma kwenye...chini ya mitini kule nyuma, mahali fulani, akiangalia kichaka chake.”

⁹⁸ Huyo akauzunguka mlima, mpaka akaufikia ule mtini mdogo, naye huyo hapo Nathanaeli amepiga magoti akiomba, sikilizeni, na kwa kuwa alimwona akiomba, kama Mkristo mwungwana alingojea mpaka akamaliza kabla kamwe hajasogea karibu. Naye akangojea mpaka huyo mtu alipomaliza kuomba, basi alipokuwa akisimama na kupangusa vazi lake, yeye, upesi sana, akasema, “Njoo, umwone Yule tuliyemwona, Yesu wa Nazareti, mwana wa Yusufu.”

⁹⁹ Sasa, mnajua mtu huyu alikuwa mwaminio wa kiothodoksi. Naye akasema...Sasa, ninaweza kumwazia akisema hivi: “Filipo, najua wewe ni mtu mzuri, hakika umeingia wazimu. Unataka kuniambia kwamba Yesu wa Nazareti, mwana wa Yusufu! Laweza neno lolote jema kutoka Nazareti?”

¹⁰⁰ Mwajua, nafikiri alimpa jibu zuri sana ambalo mtu yeyote angeweza kutoa, “Njoo uone.” Hakusema, “Kaa nyumbani na ukosoe” Ama, “Amka utoke.” Alisema, “Njoo, ujionee mwenyewe.”

¹⁰¹ Hao wakazunguka mlima, naweza kuwazia Filipo akimwambia, “Loo, unajua yule mzee aliyetuuzia samaki tangu wakati ule, jina lake Simoni?”

“Naam.”

¹⁰² “Vema, alikuja mbele ya Masihi hivi majuzi, naye Masihi akamwambia, ‘Jina lako ni Simoni.’ Unakumbuka, hata hakuwa na elimu ya kutosha kuandika jina lake mwenyewe.” Biblia ilisema ya kwamba Petro yule aliyekuwa na funguo za Ufalme, alikuwa asiye na elimu wala maarifa. Hata asingeweza kuandika jina lake mwenyewe, hakuwa na elimu kabisa. Lakini ilimpendeza Mungu kwa imani yake, kumpa funguo za Ufalme, kwa kuwa alikuwa na ufunuo wa Yesu Kristo, mtu asiye na elimu, asiye na maarifa.

¹⁰³ Naye akasema, “Alimwambia, yeye alikuwa ni nani na baba yake alikuwa ni nani. Sasa, Nathanaeli, unajua ya kwamba Masihi anapaswa kuwa Nabii aliyetumwa na Mungu. Mungu anapaswa kuwa ndani ya Masihi, kwa sababu Yeye atakuwa Mfalme wa manabii. Lakini inampasa kutupa ishara ya Masihi, kulingana na Maandiko. Na kama Mtu huyu angefanya hivi, hivi hungeamini Yeye alikuwa ni Nabii?”

¹⁰⁴ Ninaweza kuwazia Nathanaeli akisema, “Sasa, ngoja kidogo tu, Filipo. Hatujawa na nabii kwa mamia na mamia ya miaka. Basi huyu Mgalilaya anawezaje, Mtu huyu wa Nazareti anawezaje, hatuna kumbukumbu Yake shuleni wala mahali popote ambapo amekuwa, angewezaje kufanya jambo kama hilo?”

“Njoo tu, uone. Njoo, ujionee mwenyewe, uone kama inaendelea au la.”

“Nilisikia habari za yule mtu wa mwituni kule chini, Yohana.”

¹⁰⁵ “Vema, alikuwa tu ni mtangulizi, huyo alikuwa ni Isaya aliyekuwa mtangu-...na—nabii aliyekuwa aje akimtangulia. Lakini Yeye ni—Yeye ni...Sasa, huyo ndiye Eliya aliyekuwa aje; sasa, Huyu ndiye Masihi, kwa sababu Yeye huonyesha ishara ya Masihi.”

¹⁰⁶ Na kama hiyo ilikuwa ndiyo ishara ya Masihi jana, ni ile ile leo, ama Yeye alifanya ishara mbaya. Ndipo basi Israeli walikuwa sahihi, na kuhesabiwa haki kwa kumwua, wakimkana kuwa ni Masihi, maana Yeye angekuwa ni laghai. Lakini walimwua kwa sababu alithibitisha ya kwamba Yeye alikuwa ni Masihi. Hakukuwako na—hakukuwako na mwamba wa kupinduliwa, tutakapolifikia mbele zaidi katika juma mtaona. Yeye ndiye Masihi.

¹⁰⁷ Sasa, ninamwazia akisema, “Unajua, Filipino, nita—ninataka kukuamini, bali si—siwezi kabisa kufanya hivyo, kamwe siwezi kuamini kwamba jambo kama hilo limetukia. Ni nzuri sana huwezi kuamini.”

¹⁰⁸ “Vema, unajua, mimi...” Huenda Filipino alisema hivi, “Nathanaeli, halingenishangaza, ila akinambia...akikwambia wewe ni nani utakapokuja huko.”

“Loo, kamwe halitendeki hivyo. La, siliamini; itanibidi kuliona kwanza.”

¹⁰⁹ Kwa hiyo wakaja, hatimaye wakafika mkutanoni ambapo Yesu alikuwa, na labda huenda aliingia kwenye mstari wa maombi, sijui, huenda alikuwa ameketi nje kwenye kusanyiko, ama popote pale, walikuwa upande gani, wameketi chini au wamesimama. Lakini mara macho ya Yesu yalipomtazama, sikilizeni, Yeye alisema, “Tazama Mwisraeli kwelikweli, ambaye hamna hila ndani yake!” Huyu alikuwa ni Yesu jana. Hiyo ni kweli? “Tazama Mwisraeli kwelikweli, ambaye hamna hila ndani yake!”

¹¹⁰ Basi alimshangaza sana mtu huyo, hata akasema, “Rabi, ulipata kunijua lini?” Kwa maneno mengine, “Hii ndiyo mara ya kwanza tuliyouwahi kukutana. Ulijuaje kwamba nilikuwa mtu mwaminifu, mtu mwenye haki, Mwisraeli?” Si kwa jinsi alivyokuwa amevalia, watu wote wa mashariki walivalia vile vile, ndevu, na kilemba, na vazi refu, na kadhalika, ngozi nyeusi. “Ulinijuaaje?”

¹¹¹ Sikilizeni Maneno Yake: “Kabla Filipino hajakuita, ulipokuwa chini ya mti, nilikuona.” Huyu alikuwa ni Yesu jana, hivyo ndivyo alivyojidhihirisha Mwenyewe.

Alisema nini? “Rabi, Wewe ni Mwana wa Mungu, Wewe ni Mfalme wa Israeli.”

¹¹² Yesu alimwambia na kusema, “Kwa sababu nilikwambia hivi unaamini? Utaona makubwa zaidi.” Yeye ni mwaminio, aliyekusudiwa Uzima wa Milele, kuona kazi za Mungu.

¹¹³ Loo, kulikuwako na wengine waliosimama pale, hawakuamini hilo. Marabi wa siku hiyo, walisimama pale, walijua iliwabidi kuwajibika kwa kusanyiko lao, hapakuwapo na njia ya kuliepukia, watu wamesimama pale na kuliona likitendeka, nao walijua Maandiko yalifundisha hivyo ndivyo Masihi atakavyokuwa, kwa hiyo iliwabidi kuwajibika kwa watu.

¹¹⁴ Walisema nini? Kamwe hawakulisema kwa sauti, bali mioyoni mwao walisema, “Mtu huyu ni Beelzebuli, mpiga ramli, pepo fulani mchafu.” Mnaona? “Yeye ni mkuu wa pepo, mpiga ramli, na hivyo ndivyo anavyofanya mambo haya ni kwa kuagua kwake.”

¹¹⁵ Yesu alisema nini? Alisema, “Nitawasamehe hilo, lakini siku moja, Roho Mtakatifu atakuja, na kusema neno moja dhidi ya Hilo, halitasamehewa katika ulimwengu huu, wala ulimwengu ujao.” Mnaona mahali tunapojiweka basi!

¹¹⁶ Kuita...Kumkufuru Roho Mtakatifu ni nini? Kumwita Roho wa Mungu, ambaye alikuwa akifanya yale hasa Biblia ilitabiri angefanya, nguvu za pepo. Hakuna msamaha kwake, wala ulimwengu huu, wala ule ujao. Naye Yesu hawezi kusema uongo, kwa sababu Yeye alikuwa ni Mungu, na haiwezekani kwa Mungu kusema uongo. Mungu alikuwa ndani Yake, Yeye alisema, “Si Mimi, ni Baba Yangu anayeishi ndani Yangu.” Mwana alikuwa ni huyo Mtu, Mungu alikuwa ni yule Roho aliyekuwa ndani Yake, na ilikuwa ni Roho akinena kutoka Kwake.

¹¹⁷ Sasa, mnaona kile alichowafanyia hao Wayahudi? Alipokutana nao, hao waliokuwa wamekusudiwa Uzima walitambua. Msilikose enyi kanisa! Wale waliokusudiwa Uzima walilitambua na kuliadini. Lakini wale ambao hawakuamini waligeuzwa waende kwenye upotevu. Hivi Yesu hakuwambia hao watu watakatifu, waliotakaswa, walioyajua Maandiko kutoka A hadi Z, au waliodai kuyajua, Akasema, “Ninyi ni wa baba yenu ibilisi”? Hiyo ni kweli kabisa.

¹¹⁸ Kwa hiyo usiweke dhambi juu ya kuvuta sigara, kunywa pombe, kucheza kamari, hizo si dhambi, hizo ni sifa za kutokuamini, dhambi ni kutokuamini. Huenda kamwe usiiguse sigara, kunywa pombe, au kamwe usifanye uovu wowote maishani mwako, kama huamini Neno la Mungu, ungali ni mwenye dhambi. Dhambi ni kutokuamini. Kuna roho mbili tu, mmoja anaamini, na huyo mwingine haamini.

¹¹⁹ Haidhuru...Tumeweka msingi mawazo yetu yote juu ya namna fulani ya tendo takatifu, jambo tunalotaka kufanya, na

jambo ambalo tulifanya, “Niliwapa akina Jones makaa kidogo, wakati walipokuwa . . . Nina haki ya kwenda Mbinguni.” Huna haki yoyote ya kwenda Mbinguni, mpaka utakapomwamini Mungu, na kulikubali kwa msingi wa imani juu ya Damu iliyomwagika ya Yesu Kristo, Mwana wa Mungu.

¹²⁰ Huna haki, kwa maana hakuna njia nyingine, haidhuru, huenda ukawa mfuasi hodari, Mpentekoste kwelikweli, Mmethodisti, Mbaptisti, ama Mkatoliki kwelikweli, haileti tofauti wewe ni wa kanisa gani, kama umemwamini Yesu Kristo kwa uchaji, na kumkubali kama Mwokozi wako binafsi, kama imani yako Kwake, sijali unahudhuria kanisa gani, umeokolewa kwa imani. Na bila hiyo, kuna . . .

¹²¹ Hakuna kanisa takatifu, hakuna watu watakatifu, ni Roho Mtakatifu ndani ya hao watu, ndiye anayelifanya takatifu. Mungu Mtakatifu anayeishi miongoni mwa watu, ndiye anayeufanya huo utakatifu. Si jambo ninalofanya, jambo unalofanya, ama jambo ambalo tungekuwa tumefanya, bali ni yale ambayo Mungu ametufanyia, kupitia Kristo Yesu, hiyo ni Biblia.

¹²² Waangalie Wayahudi, waliamini kwa uchaji, baadhi yao, waliokuwa wamekusudiwa uzima; wengine, wenye msimamo thabiti katika imani zao, zilizoungwa mkono na watu wengi, hata wasingewapata na doa, wao walikuwa, ilibidi waje kupitia ukoo wa ukuhani, chini, chini, chini, chini, kutoka kwa babu hadi kwa babu na babu, ili kuwa Mlawi, kuwa mwalimu, lakini walikuwa wamefundishwa katika mapokeo, badala ya Neno halisi.

¹²³ Yesu alisema, “Ninyi ni . . . baba . . . Baba yenu ni ibilisi.”

¹²⁴ Lakini maskini hao wavuvi wadogo, wanyenyekevu, ambao wangepokea na kuamini, ambao walikuwa wamefundishwa na kujua hivyo ndivyo Masihi angekuwa, walilitambua wakati walipoliona na kuliadini, kasema, “Hakika Wewe ni Mwana wa Mungu, kweli, Rabi, tunajua ya kuwa Wewe ni Mwalimu umetoka kwa Mungu.”

¹²⁵ Nikodemo alilielezea vizuri, kanisa halingemruhusu kulipokea, lakini hata hivyo, alitaka . . . “Tunajua ya kwamba Wewe ni Mwalimu, umetoka kwa Mungu, maana hakuna mtu angeweza kufanya mambo uyafanyayo Wewe, isipokuwa Mungu yu pamoja Naye. Tunajua haliwezi kukosea, Wewe ndiwe Masihi, ulituyonesha ishara Yako ya kwamba Wewe ni Masihi. Tunajua Musa alinena ya kwamba Wewe ungekuja, tunajua Maandiko yanasema Wewe ungekuja, tunajua ya kwamba Wewe ulikuwa uwe Mungu-Nabii. Nawe huyu hapa ukituthibitishia, hata ukiyajua mawazo yaliyo moyoni mwetu. Tunajua Wewe ni Mwalimu, unatoka kwa Mungu.”

¹²⁶ Sasa, Yeye huja tu kwa wale wanaomtazamia. Sisi Wamataifa, Waanglo-Sakson, katika siku hizo tulikuwa

makafiri, Warumi, na kadhalika, tulikuwa na rungu mgongoni mwetu na kuabudu sanamu. Lakini kulikuwako na tabaka lingine la watu ambalo lilikuwa ni Wasamaria, walikuwa nusu Myahudi na Mmataifa, basi walikuwa wakimtaamia Masihi. Sasa, upesi sasa, tuna kama tu dakika tano zaidi. Walikuwa wakimtaamia Masihi.

¹²⁷ Naye Yesu alikuwa akienda zake Yeriko, bali alihitaji kupitia Samaria. Sijui ni kwa nini. Sasa, sikilizeni kwa makini sana. Ndipo alipofika kwenye mji fulani, aliwatuma wanafunzi wake kununua vyakula, Naye Mwenyewe akaketi kando ya kisima. Kama uliwahi kuwa kule, ni mandhari, kisima bado kipo, kitu tu kama hiki hapa, si kirefu sana, kimezungukwa na mizabibu, kisima cha umma ambapo watu walikuja kuchota maji yao. Kina mama walikuja huko nje na kuchukua madumu haya makubwa yaliyojaa maji bado, wakayawekelea vichwami mwao, na kutembea vizuri tu upendavyo, na kuzungumza kama wanawake wawezavyo, mwajua, wakizungumziana, na kuendelea moja kwa moja pasipo kumwaga hata tone lake moja. Nao wakaja pale kuchota maji yao.

¹²⁸ Yesu aliketi chini kwa sababu alikuwa amechoka, kama alivyosema. Nao wanafunzi wakaenda mjini kununua chakula. Basi walipokuwa wameondoka, akatokea msichana mwenye sura nzuri, ambaye alikuwa ni mwanamke mwenye sifa mbaya. Alikuwa ametia unajisi nadhiri za ndoa, alikuwa ameolewa mara tano, naye alikuwa akiishi na mume wake wa sita.

¹²⁹ Hebu tuseme alitoka, katika siku hizo, ukweli wake halisi ni kwamba, asingeweza kuambatana na hao wanawake asubuhi na mapema, kwa sababu hawakushirikiana pamoja, wema na wabaya. Siku hizi wote wamechanganyikana, huwezi kuwatofautisha, wanavaa sawa, wanafanana, wanazungumza sawa, kitu kile kile tu, wote wanavuta sigara, na wanatoka nje na kufanya yasiyofaa, wanakata nywele zao, na kutumia vipodozi, nawe huwezi. . . katili kabisa. Haya basi. Hawa hapa wanakuja.

¹³⁰ Na kwa hiyo akaja kisimani baada ya wanawake wengine wote kuondoka, naye akaanza kushusha ninii. . . ni winchi, nao wana kulabu, ninii kubwa. . . kwa kweli si ndoo, ni—ni chungu, ama kitu kama birika, kina shingo ndefu juu yake, kina kulabu mbili. Nao wakaweka hi—hiyo winchi chini ya hizi zinazoonekana kama mikono, na kukishusha ki—kisimani, na kuchota maji, kisha kukivuta juu tena.

Kwa hiyo wakati alipoanza kushusha hi—hicho chungu kisimani, akamsikia Mwanamume akisema, “Mwanamke, nipe maji ninywe.”

¹³¹ Ndipo akaangalia na kuona Myahudi ameketi pale. Loo, Yeye alikuwa tu na umri wa miaka thelathini na mitatu, lakini hapana shaka alionekana kama ana hamsini hivi, kwa sababu ndio kwanza wamwambie a—alionekana mwenye umri wa miaka

hamsini, kwa vyovyote vile, kasema, “Wewe hujapata bado zaidi ya miaka hamsini, na unasema ati umemwona Ibrahimu?” Mnaona? Kwa hiyo hapana shaka kazi Yake ilimvunja moyo sana.

Kwa hiyo huyo hapo ameketi karibu na kisima, kasema, “Mwanamke, nipe maji ninywe.”

¹³² Ndipo akaangalia kote, na akamjulisha kwamba kulikuwako na ubaguzi katika nchi hiyo. Akasema, “Tuna- . . . Wewe ni M—Myahudi, nami ni mwanamke Msamaria, Hamna desturi kama hizo hapa, za kuniuliza kitu kama hicho.”

¹³³ Angalieni hilo swali likirudi. “Lakini kama ungaliuja,” Ee Mungu, “kama ulijua ni Nani unayesema naye, ungeniomba Mimi maji unywe.” [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] “. . . maji ya Uzima, yakibubujika.” Kwa hiyo swali likazuka kuhusu kuabudia mlimani, ama Yerusalemu.

¹³⁴ Yesu alikuwa akifanya nini? Sasa, Yeye alikuwa na haja kupitia Samaria, Naye alisema hakufanya lolote mpaka Baba alipomwonyesha, basi alikuwa na haja ya kupitia kule, Baba alikuwa amemtuma huko juu. Na hapana shaka, Yeye alisema, katika Yohana Mtakatifu 5:19, “Sifanyi lolote mpaka nimwone Baba akilitenda, Baba ananionyesha kwanza, katika ono, la kufanya.” Ni wangapi waliopata kusoma Maandiko hayo, Yohana Mtakatifu 5:19? Naam, “Sifanyi neno lolote mpaka nimwone Baba analitenda kwanza, ndipo natenda tu kile Yeye anachionyesha kutenda.”

¹³⁵ Ndipo akaona jambo hili likiendelea, na hapana shaka alimwona yule mwanamke akija, bali ilimbidi kumhoji, alikuwa akijaribu kuipata roho yake. Mnaona? Kwa hiyo, Yeye akasema, hiyo ndiyo sababu Yeye alisema, “Nipe maji ninywe.” Alijua kwa ono hivyo ndivyo alivyoonekana, yule mwanamke, kwa hiyo alijua alipaswa kuonekana hivyo. Na, labda, labda mawimbi yake yote ya nywele yakining’inia chini usoni mwake, naye hakuonekana wa kupendeza sana, lakini hata hivyo, alikuja kuteka maji, ndipo Yeye akaanza kuzungumza naye. Naye akasema . . .

¹³⁶ Akasema, “Inatupasa kuabudu katika mlima huu, na—nao baba zetu waliabudia hapa, naye baba yetu, Yakobo, unaona, yeye ndiye aliyechimba hiki kisima.” Na—nao walijua Mungu alikuwa ni Mungu, pia, walikuwa wakimtazamia Masihi kuja, nao wakasema, “Nawe unasema huko Yerusalemu . . .”

¹³⁷ Akasema, “Saa imekuja na sasa ipo, ambapo hamtaabu- . . . hamtaabudia Yerusalemu, wala katika mlima huu. Lakini Mungu ni Roho, nao wamwabuduo Yeye imewapasa kumwabudu katika Roho na Kweli.” Swali likaendelea, wakaendelea, akizungumza naye mpaka alipoishika roho yake.

¹³⁸ Sasa, nilisema sina budi kuthibitisha mambo yote kwa Neno la Mungu. Sasa, papo hapo nisingeweza kuthibitisha hilo

kwa Neno, lakini kwa... Kama mngeninii... Ilibidi iwe hivyo, kwa sababu Yeye alikuwa akizungumza naye. Mnajua Yeye alizungumza naye, Naye akaishika roho yake, Naye akapata kujua shida yake ilikuwa wapi. Ni wangapi wanaojua shida yake ilikuwa ni nini? Hakika, alikuwa akiishi... alikuwa na waume sita.

¹³⁹ Naye akasema, “Mwanamke, nenda kamwite mumeo, mje naye hapa.” Sasa, angalieni, Yeye ana... Huyu ni Masihi, mnaamini Yeye alikuwa ni Masihi? “Nenda, kamwite mumeo, mje naye hapa.”

¹⁴⁰ Akaenda, akasema, “Sina mume.” Loo, ni kukanushwa vibaya jinsi gani kwa yale aliyokuwa amesema!

Akasema, “Umesema kweli. Umekuwa na waume watano, na yule unayeishi naye sasa siye mume wako, kwa hiyo umesema kweli.”

¹⁴¹ Mwangalieni mwanamke huyo, angalia jinsi alivyomjua Mungu zaidi ya vile hao makuhani walivyomjua. Wazia jambo hilo, ndugu. Hao makuhani walisema, “Yeye ni Beelzebuli, mpiga ramli.”

¹⁴² Mwanamke huyo alisema nini? Alisema, “Bwana, naona ya kuwa Wewe ni Nabii. Tunajua, sisi Wasamaria tunajua ya kwamba Masihi ajapo, hiyo itakuwa ndiyo ishara Yake, Atatwambia mambo haya ajapo Masihi. Tunajua Masihi, anayeitwa Kristo, Mtiwa mafuta, atakapokuja, Yeye atatuambia mambo haya, lakini u Nani Wewe?”

Akasema, “Mimi ninayesema nawe Ndiye.” Loo, jamani!

¹⁴³ Akaangusha mtungi wake wa maji, akakimbia mjini na kusema, “Njoni, mwone Mtu aliyeniambia mambo ambayo nimefanya. Haimkini Huyu kuwa ndiye Masihi?”

¹⁴⁴ Nayo Biblia ilisema, “Watu wa mji ule walimwamini kwa ajili ya neno la mwanamke huyo.” Hiyo ni kweli, enyi walimu wa Biblia? Kwa sababu ya neno la yule mwanamke, walimwamini. Huyu alikuwa ni Yesu jana. Hivyo ndivyo alivyojitambulisha Mwenyewe, Wayahudi na Wasamaria pia, lakini si kwa Mataifa, hakuna hata wakati mmoja jambo hilo lilitendwa mbele ya Mmataifa. Lakini Yeye alitabiri na kusema wakati wa jioni jambo hilo lingekuja.

¹⁴⁵ Mnasema, “Ni wapi, Ndugu Branham?” Vema, nitawapa katika Andiko moja sasa hivi, kama kufunga, Yesu alisema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu.” Hiyo ni kweli?

¹⁴⁶ Hebu na tuchukue Sodoma, tuone kile alichofanya. Huko Sodoma, Lutu alikuwa amejitenga mwenyewe, mwaminio vuguvugu, naye alikuwa ameshuka kwenda Sodoma, naye alikuwa amejijengea sifa nzuri huko chini. Lakini Ibrahimu

alika nje ya Sodoma, na kuishi kulingana na ahadi ambayo Mungu alikuwa amempa.

¹⁴⁷ Sasa, daima, kuna matabaka matatu ya watu, kila mkutano unao, kila mji unao, kila kanisa linao, hao ni wasioamini, wanaojifanya waaminio, na waaminio. Hiyo ni kweli kabisa. Daima imekuwa hivyo, ingalipo hata wa leo, kila kusanyiko, kila mkusanyiko wa pamoja, hata wakati wana wa Mungu walipokuja mbele za Mungu, alikuwapo.

¹⁴⁸ Kwa hiyo tunaona hapa ya kwamba katika mfano wa Sodoma... Sasa, angalieni jinsi alivyosema hili kwa makini, jinsi alivyolisema, jinsi alivyolitamka. Mnaona? Na Sodoma ilikuwa tu kabla ya ule Moto kushuka. Mnaona? Na huo ndio unaokaribia kushuka sasa, Moto. Tunajua hilo. Huu ni ulimwengu uliohukumiwa, tunajua hilo, ha—hauna tumaini, bila Mungu, umepotea, ni masalio machache tu ya watu walio tayari kwa ajili ya Unyakuo. Juma hili, Mungu akipenda, nitathibitisha hilo, neno kwa neno. Angalieni, sisi ni watu waliohukumiwa, ama, ulimwengu umehukumiwa, Kanisa halijahukumiwa. Namshukuru Mungu kuna masalio.

¹⁴⁹ Angalieni, lakini sasa angalieni ishara ya mwisho ambayo Sodoma ilipokea. Yeye alikuwa pamoja na Ibrahimu wakati wote, lakini siku moja, kabla tu ya kuteketezwa kwa mji wa Sodoma na Gomora, tunaona ya kwamba wanao wapotovu wengi sana huko chini. Angalieni mataifa siku hizi. Mnaona? Kila wazo moyoni mwa mwanadamu lilikuwa ovu, hata walikuwa wakijipotosha katika mambo ya kujuana kimwili, kadhalika.

¹⁵⁰ Angalieni, kulikuwa na watatu waliokuja kumlaki Ibrahimu, walionekana kama wanadamu, mavumbi nguoni mwao, na kukiri kwamba walikuwa wageni. Ndipo wawili kati yao wakashuka kwenda kuhubiri Sodoma, wakijaribu kupata watu kumi. Kumbukeni, walishuka kwenda Sodoma, kanisa vuguvugu, Billy Graham wa kisasa, na kadhalika, huko chini Sodoma, wakihubiri Injili, wakiwapofusha watu kwa Injili.

¹⁵¹ Hivyo ndivyo mwinjilisti Billy Graham, na Oral Roberts, na wengi wa hao watu mashuhuri wa Mungu wamefanya, wamewatikisa watu, taifa hili limetikiswa. Ulimwengu unajua habari zake, kwa huduma kuu ya watu hawa waliotolewa na Mungu, wameyatikisa mataifa kwa huduma yao.

¹⁵² Lakini kumbukeni, neno *kanisa* linamaanisha, “walioitwa watoke.” Ibrahimu alikuwa amejitenga na upuuzi huo wote. Kwa hiyo, Yule aliyebaki nyuma na kuzungumza na Ibrahimu, ambaye Ibrahimu alimwita, Bwana, huyo alikuwa ni Mungu. Ninajua huenda msikubaliane na hilo, lakini angalieni yale Maandi... Ibrahimu ndiye aliyekuwa akizungumza Naye, alimwita, herufi kubwa B-w-a-n-a, Elohimu, “Bwana Mungu.” Alikuwa akifanya nini? Ibrahimu alimlisha nyama ya ndama,

maziwa ya ng'ombe, siagi, na keki, Naye akala; Naye alikuwa Elohimu. Yesu alirejeaje hilo?

¹⁵³ Sasa angalieni, siku chache kabla ya hapo, Mungu alikuwa amebadilisha jina la Ibrahimu, ama, Abram, likawa Ibrahimu; S-a-r-r-i, likawa S-a-r-a-h, Sarah, "binti mfalme." Ibrahimu, alimpa sehemu ya Jina Lake, *Elohimu*, Ibrahimu, kama baba wa mataifa.

¹⁵⁴ Basi mwangalieni Huyu aliyeketi na kuzungumza naye, Mtu, aliyevaa nguo, mavumbi juu yao, akila nyama kama tu mwanadamu mwingine yeyote, Yeye alisema, "Ibrahimu, yu wapi Sara, mkeo?" Angalieni Maandiko.

Ibrahimu akasema, "Yuko hemani nyuma Yako."

¹⁵⁵ Akasema, "Nitakuzuru." Hilo lilithibitisha kile alichokuwa. "Nitakuzuru kulingana na ahadi Yangu niliyokupa. Nitakuzuru, nawe utampata mtoto huyu mchanga, ambaye umemngojea miaka ishirini na mitano, yeye ana tisini, nawe una mia moja sasa, kwa hiyo nitakupata mtoto huyo mchanga."

¹⁵⁶ Ndipo Sara akacheka moyoni mwake kimoyomoyo, ilisema Biblia, huku Malaika ameelekeza mgongo Wake kwenye hema. Kisha kasema, "Mimi, mwanamke mkongwe, nipate raha na bwana wangu huko nje, naye ni mkongwe, pia?"

Ndipo yule Malaika huku ameugeza mgongo Wake, Mungu aliyedhihirisha katika mwili, kasema, "Kwa nini Sara akacheka, akisema moyoni mwake...?"

¹⁵⁷ Yesu alisema nini? "Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu." Jambo lilo hilo, Mungu akidhihirishwa katika mwili wa watu Wake, sio Malaika wakishuka, bali wanadamu, waliozaliwa na Roho wa Mungu, wakiwa na Uzima wa Milele kifiani mwao, wakitenda na kufanya jambo lile lile ambalo Malaika alifanya kule Sodoma.

¹⁵⁸ "Mabwana, sisi tunataka kumwona Yesu." Kama Yeye yu hai leo, na alikuwa katika kanisa hili, angefanya vile vile alivyofanya wakati huo. Nako huku ni kumalizia kwa wakati wa Mataifa. Nabii alisema, "Kutakuwako na siku, ambayo haingelitwa mchana wala usiku, lakini wakati wa jioni itakuwa Nuru."

¹⁵⁹ Sasa, jua, kijiografia, huchomoza mashariki na kutua magharibi, jua lile lile. Vema, sasa, wakati M-w-a-n-a alipochomoza juu ya watu wa mashariki na kuonyesha nguvu Zake za kimiujiza... Tumekuwa na siku, imekuwa siku yenye utusitusi, yenye mvua, tumekuwa na Nuru ya kutosha hata tungeweza kujiunga na kanisa, kujenga madhehebu, na kuwa na wakati mzuri sana, kuwa Wakristo, kumkubali Kristo, lakini hiyo Nuru ya Mwana haijawahi kumiminika tangu wakati huo. Lakini hii ni...

¹⁶⁰ Ustaarabu umesafiri pamoja na jua. Ustaarabu wa kale kuliko wote ni Uchina. Tumekuja... Limesafiri kutoka mashariki, likija magharibi pamoja na jua, tuko kwenye Pwani ya Magharibi sasa. Nayo Biblia ilisema, nabii alisema, "Itakuwa Nuru wakati wa jioni." Mwana yuyo huyo aliyechomoza mashariki atakuwa akiangaza kwa nguvu Zake zile zile juu ya watu wa magharibi kama alivyofanya huko mashariki. "Mabwana, sisi tunataka kumwona Yesu." Kwa nini tusiweze kumwona? Kwa nini tusiweze kumwona, wakati Yeye aliahidi jambo hilo?

Mnasema, "Ndugu Branham, hiyo ni Biblia, lakini je, itafanya kazi?"

¹⁶¹ Kama ni ahadi ya Mungu itatenda kazi, haina budi kutenda kazi. Mnaamini hilo? Kama angekuja kwenye kusanyiko hili la watu usiku wa leo, na kufanya, na kufanya jambo lile lile alilofanya alipokuwa hapa wakati huo, kumjulisha, kukujulisha, ya kwamba Yeye yupo hapa, Kristo yeye yule, angefanya jambo lile lile, mngemwamini? Inueni mikono yenu na kusema, "Ningeamini, kama ningeweza kuliona likitendeka."

Na tuinamishe vichwa vyetu.

¹⁶² Mungu Mwenyezi na Mwenye nguvu zote, tunakushukuru, Ee Baba Mtakatifu, kwa ajili ya ahadi uliyotupa, nasi tunajua ya kwamba ahadi Zako ni kweli. Sasa, ni usiku mbaya nje, lakini ndani ni usiku mtukufu, si usiku ndani, bali siku ambapo Mwana wa Mungu anaangaza mioyoni mwetu na maishani mwetu. Tunakushukuru kwa ajili ya waaminio, na kwa ajili ya Kristo aliyeahidi kuja kwa waaminio hawa, na kujidhihirisha Mwenyewe, na kujionyesha katika siku hizi za mwisho kwa jamii ya Mataifa, ambalo tunajua, Baba, halijawahi kuwako kulingana na historia tangu kanisa la mwanzoni lilipofikia, mpaka wakati huu, jinsi Mtakatifu Paulo na hao katika siku za kale, jinsi ambavyo maono yaliwatokea, nao wakafanya jambo lile lile, Anania na Safira; na Paulo juu ya bahari usiku ule; naye Malaika wa Bwana akasimama karibu naye, naye akatoka na kuwaambia watu; na jinsi ambavyo zile nguvu kuu za Mungu zilivyojulikana katika kanisa hilo la mwanzoni, uliahidi jambo hilo tena katika siku za mwisho.

¹⁶³ Ninaomba, Baba, ya kwamba utayasamehe makosa ya mtumishi Wako. Na sasa, jalia Roho Mtakatifu aje, kwa sababu ni Neno Lake, na jalia afanye mbele ya watu hawa, nikiisha kuwaambia, Baba, kwamba wokovu ni yale ambayo wamefanyiwa tayari pale Kalvari, uponyaji wa Kiungu ni yale uliyowafanyia pale Kalvari.

¹⁶⁴ Nami nakuomba Wewe, Bwana, kwamba wapate kuelewa ya kwamba ni imani yao wenyewe. Ndipo wanapomwona Mungu aliyetoa ahadi akija katika nguvu Zake na kufanya kama alivyofanya wakati huo, watajua ya kwamba ni Yesu yeye

yule aliyetoa ahadi. Tujalie, Bwana, tunapojikabidhi Kwako, na kusanyiko hili, kwa ajili ya Ufalme wa Mungu. Katika Jina la Yesu Kristo, tunaomba. Amina.

¹⁶⁵ Sasa nitautiliza kama kuna mtu yeyote hapa, ambaye anataka kuondoka katika dakika kumi hadi kumi na tano zijazo, kwamba uondoke sasa, kusudi usiisumbue ibada. Sasa, sasa tafadhalini msisogeosogee huku na huku tangu sasa, mnaona, baada ya dakika hii, kaeni tu vitini mwenu.

¹⁶⁶ Kila siku ambayo tutakuwa na maombi kwa ajili ya wagonjwa... Nitazungumza hili, wakati mtu fulani hana budi kuondoka, lakini kama mnaweza, ngojeni dakika zingine kumi na tano, kuangalia na kuona kama Neno ni kweli. Sasa, mtu yeyote anaweza kuja, aseme hivyo, lakini sasa inahitaji Mungu kulifanya litende kazi. Hiyo ni kweli. Inahitaji... Sasa, kama...

¹⁶⁷ Kila siku tunapowaomba wagonjwa usiku, tutashuka, na—nao hao wavulana watasambaza kadi za maombi. Ama itakuwa ni mwanangu, Billy Paul; mvulana huyu papa hapa, Gene Goad, ambaye ni mmoja wa vijana wa kanda; na kuna mwingine anayeitwa Leo, Leo Mercier; mmoja wa hao wavulana atasambaza kadi.

¹⁶⁸ Watasimama mbele ya kusanyiko na kuchanganya kadi zote pamoja, ndipo watashuka waje na kukupa kadi ya maombi. Kwa hiyo hawajui ni kadi ya namna gani ya maombi wanayowapa watu, kwamba ni nani atakayeitwa, ni nani hataitwa, hilo linawahesabia haki, wala hakuna ajuaye, tena, mahali watakapoanzia mpaka usiku huo, wakati Roho Mtakatifu anapoliweka moyoni mwetu, popote pale. Bila shaka, hilo halina uhusiano wowote na kuponywa kwa watu, bali ni kumleta tu mtu fulani hapa jukwaani mbele ya Roho wa Bwana.

¹⁶⁹ Halafu basi, ninyi huko nje kwenye kusanyiko msio na kadi ya maombi, msichoke, ketini hapo na mwamini kwa moyo wenu wote, mwangalie kinachotukia. Sasa, natumaini mtasikiliza mambo ambayo nimesema, kwamba hamtatembea—tembea huku tena.

¹⁷⁰ Na, tafadhalini, mtu asipige picha wakati huu, kwa sababu baadaye kidogo, ninaweza kuwaambia ni Nuru, yule Malaika wa Bwana, sote tunajua alikuwa ni Nguzo ya Moto, tulikuwa na picha Yake hapa kutoka Ujerumani, kutoka Uswisi, kutoka Marekani, kutoka mbele ya FBI, na zote zimethibitishwa, ni Kiumbe cha kimbinguni, atakuwa jukwaani katika dakika moja. Na ni Roho yule yule wa Mungu, hasa. Kwa hiyo msipige picha kuanzia sasa, kuanzia sasa na kuendelea, kote ibadani, na mketi, na mwe na kicho sana, na watulivu, wakati watu wakija.

¹⁷¹ Sasa, ninaamini... Ulininii? Ama, Billy, ulisambaza...? Huh? Ati nini? Moja hadi mia moja? Vema, muda umeenda hivi, hatutaweza kuwaita wengi mno. Lakini zishikilieni kadi zenu. Hebu tuwaite watu wachache hapa juu.

¹⁷² Ni nani aliye na kadi ya maombi namba moja? Kama unaweza kusimama, ama kuinua mkono wako. Kadi ya maombi namba moja. Ni—ni herufi gani iliyoandikwa juu yake? A, A, namba moja. Mtu yeyote aliye nayo? Je, utaninii...? Lazima kuna kasoro mahali fulani. Vema, tutaanza... Loo, samahani, sawa. Waweza kuja papa hapa, mama? Namba mbili. Kadi ya maombi A, namba mbili. Inua mkono wako. Vema. Njoo papa hapa, mama. Namba tatu, waweza kuinua mkono wako? Vema, namba tatu. Je, niliiona? Naam, huko nyuma kabisa. Namba nne, waweza kuinua mkono wako? Huko nyuma kabisa, sawa. Namba...

¹⁷³ Vema, yeye huzisambaza popote pale jengoni, mtu yeyote anayezitaka. Namba tano. Waweza kuinua mkono wako, yeyote aliye na kadi ya maombi namba tano? Vema. Namba sita, waweza kuinua mkono wako? Inua mkono wako ili niweze kuona. Vema, bwana, papa hapa. Namba saba, namba nane, namba tisa. Ninapokuita njoo huku... Namba kumi. Hiyo ni sawa.

¹⁷⁴ Mnaona, huu huenda ukawa ni uwanja wa mpira wa vikapu, uwanja wa michezo, bali si uwanja wa michezo usiku wa leo, ni kanisa la Mungu. Mnaona? Kwa hiyo hatuna budi kuwa na uchaji na heshima kwa Roho Mtakatifu. Moja, mbili, tatu, nne, tano, sita, saba, nane, tisa. Namba kumi. Ni nani aliye na kadi ya maombi namba kumi? Vema, mama. Namba kumi na moja. Vema. Namba kumi na mbili. Namba kumi na mbili, kumi na tatu, kumi na nne, kumi na nne, kumi na nne, kumi na nne? Vema, hiyo imetosha. Hebu—hebu tuanzie papo hapo. Sasa, yeyote aliye na kadi, zishikilieni, zishikilieni tu, zitaitwa.

¹⁷⁵ Sasa, nadhani ya kwamba asilimia tisini na tisa ya kusanyiko hili, labda, hatufahamiani. Wote walio katika kusanyiko hili ambao hatufahamiani, inueni mikono yenu. Mnaona? Nadhani hapa yapata asilimia mia moja. Vema.

¹⁷⁶ Ni wangapi humu ndani wasio na kadi ya maombi, nawe ni mgonjwa, nawe unataka Mungu akuponye, huna kadi ya maombi, wala hatufahamiani, inueni mikono yenu, kila mahali humu jengoni, sijali uko wapi. Vema, hiyo ni karibu tu kwa jumla, kila mahali. Vema.

¹⁷⁷ Sasa, wakati wakiwapanga watu, ningetaka kuwaambia jambo fulani. Wakati mmoja Yesu alikuwa anaenda kumfufua msichana mdogo, aliyekufa, binti Yairo, na kulikuwa na mwanamke aliyekuwa akitokwa na damu, naye akasema moyoni mwake, “Ninaamini ya kwamba Yeye ni Masihi, ili kwamba kama ninaweza tu kugusa ukingo wa vazi Lake, upindo wa vazi Lake, nitakuwa mzima.” Ni wangapi waliowahi kusoma hadithi hiyo? Hakika. Naye akagusa vazi Lake, kwa sababu hivyo ndivyo alivyotaka kufanya. Alimwamini, hakuwa amewahi kumwona hapo kabla, bali alimwamini, mara alipomwona, alimwamini.

¹⁷⁸ Kwa hiyo basi, aligusa vazi Lake. Sasa, asingeweza kuuhisi kimwili. Vazi la Kipalestina linapwaya, nalo lina vazi la ndani, na basi Yeye asingeweza kuhisi hilo. Ndipo maskini mwanamke huyo akagusa vazi Lake, kila mtu alikuwa akipeana mikono na Yeye, na kadhalika, na kumkumbatia. Na kwa hiyo, Yeye akasema basi, huyo mwanamke alitoka akaenda kwenye kusanyiko na kuketi chini, ama chochote kile, naye akasema. . . Akasema, “Ni nani aliyenigusa?”

Ndipo Petro akamkemea, akasema, “Bwana, kwa nini ulisema jambo kama hilo?” Kasema, “Kila mtu anakugusa.”

¹⁷⁹ Akasema, “Lakini naona kwamba nimekuwa dhaifu.” La King James linasema *nguvu*, ambapo, *nguvu* ni “uweza.” “Naona kwamba nguvu zimenitoka.” Naye akaangalia kote kwenye kusanyiko mpaka akamwona maskini mwanamke huyo, na kumwambia ya kwamba alikuwa anatokwa na damu, na imani yake ilikuwa imemwokoa. Hiyo ni kweli?

¹⁸⁰ Vema sasa, kwenu ninyi watu, msio na kadi ya maombi, kama Yeye ni yeye yule jana, leo, na hata milele, si angetenda vivyo hivyo leo kama ungemgusa? Hiyo ni kweli?

¹⁸¹ Sasa, ni wangapi. . . ? Ninyi wahudumu hapa mnajua jambo hili, nanyi wahudumu, na ninyi wasomaji wa Biblia huko nje, kwamba Biblia ilisema ya kwamba Yesu Kristo, sasa hivi, ni Kuhani Mkuu anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu. Hiyo ni kweli? Sasa hivi, Yeye ni Kuhani Mkuu. Hiyo ni kweli, ndugu? Vema, kama Yeye ni Kuhani Mkuu yeye yule aliyekuwa wakati huo, angetendaje sasa? Kama Yeye ni Kuhani Mkuu yeye yule aliyekuwa wakati huo, angetenda vivyo hivyo. Hiyo ni kweli? Kwa sababu Yeye ni Kuhani Mkuu yeye yule, Yeye ni Mungu, hawezi kubadilika, hawezi kuwa tofauti na vile alivyokuwa.

¹⁸² Kama Yeye—kama akiliacha kanisa hili la Mataifa lipite bila ya kuwa na ishara ile ile ya Masihi, basi aliwafanyia jambo fulani, wale Wasamaria, na Wayahudi, ambalo hakutufanyia sisi, kwa hiyo hilo lisingekuwa la haki. Wasingeweza kufaulu kwa theolojia, iliwabidi kuwa na wakati wa kuihukumu theolojia yao, kulidhihirisha Neno la Mungu kwao katika mwili, na vivyo hivyo kanisa la Mataifa linalipata sasa.

¹⁸³ Sasa, tafadhalini, naomba tena, msi—msitembee—tembee, tafadhalini. Mnaona? Roho Mtakatifu ni mwoga tu awezavyo kuwa. Na wakati mwingine unaposogea, unaona, wewe ni roho, wewe ni nafsi, basi unaposogea, hilo linatatiza, mnaona. Kaeni tu kimya kabisa, iweni na kicho. Sasa, baada ya jambo fulani kufanywa, kama Roho Mtakatifu akifanya jambo fulani, mnataka kusema, “Bwana asifiwe,” vema, bali wakati mnapoanza kuwasiliana na Roho wa Mungu, tulieni kabisa. Iweni tu katika maombi.

¹⁸⁴ Nanyi huko nje msio na kadi ya maombi, semeni hivi: “Bwana Yesu, ninajua mtu huyo hanijui, nami ninajua yeye ni mwanadamu tu, bali ninaamini Wewe ni Mungu. Nami naamini... Amesoma Maandiko, aliniambia kweli, kwa hiyo mimi ni mgonjwa na mhitaji, jalia nikuguse Wewe, Baba.” Tafuta kujua kinachotukia. Unasema, “Sasa, Wewe nena kupitia kwake, yeye ni msemaji tu.” Angalieni, maikrofoni hii ni bubu mpaka kitu fulani kizungumze ndani yake, vivyo hivyo na mimi, simjui yeyote wenu.

¹⁸⁵ Sasa, kila mtu katika mstari huo wa maombi anayejua ya kwamba sijui lolote kuwahusu, inueni mikono yenu, kote huko, mnaojua sijui lolote kuwahusu. Mnaona? Basi hii hapa mikono yangu, najua, sijawahi kuwaona watu hao hapo kabla maishani mwangu, nijuavyo mimi. Hakuna mtu humu, ambaye nimewahi kumwona. Siwezi kumwona mtu humu jengoni nimjuaye, isipokuwa huyu awe ni rafiki msiri wangu Ndugu Skaggs kutoka Chicago, aliyeketi kwenye hii... Huyu ni wewe, Ndugu Skaggs? Nilidhani ilikuwa hapo. Nami ninajua ya kwamba kuna Ndugu Fred Sothmann, ninaamini yupo hapa mahali fulani jengoni. Na labda, Tom Simpson, nadhani, yuko hapa mahali fulani jengoni. Sijui. Uko wapi? Mko hapa, Ndugu Fred na Ndugu Tom? Niliona gari lao huko nje... Naam, wako papa hapa, huko nyuma kabisa. Vema.

Sasa, iweni na kicho kabisa. Vema, ninii... Sasa, kama watu wakichoka kidogo, wapeni kiti.

Njoo tu hapa juu, mama.

¹⁸⁶ Sasa, Hili *hapa* Neno. Ni wangapi wanaoamini ya kwamba niliwasomea, na kuwahubiria Neno la Mungu, ahadi ya Mungu? Sasa, Hili *hapa* Neno la Mungu. Sasa, huyu hapa mtu ambaye sijapata kumwona hapo kabla, je, itafanya kazi? Itafanya endapo anaamini, nami ninaamini, na ninaweza kujitolea kwa Mungu, kama vile kwa karama, na kumwachilia Yeye, nijiondoe tu, na kumwacha Yeye azungumze. Kwa hiyo kama kuna jambo lolote lililofanywa, kama ingekuwa ni Bwana Yesu, inge... mngejua haina budi kuwa ni Roho.

¹⁸⁷ Sasa, hebu tuchukue, kama tu nilivyokuwa nikinukuu dakika chache zilizopita, Yohana Mtakatifu 4, huyu hapa mwanamke na mwanamume ambao hawajawahi kukutana hapo awali, sasa, tukiwa hatufahamiani, na ni katika mandhari ndogo tu kama niliyokuwa nikizungumzia. Sasa, Yohana Mtakatifu 4, Yesu alikutana na mwanamke Msamaria, Naye akazungumza naye kwa muda kidogo, mpaka akaishika roho yake kisha akamwambia, shida yake.

¹⁸⁸ Na sasa, kama angekufanyia jambo lilo hilo usiku wa leo, ukijua ya kwamba sikujui, unaona, na Mungu anakujua, wala hunijui, ama isipokuwa unanijua tu kwa jina, ama chochote kile, lakini kama—kama Yeye angefanya jambo lile lile, je,

ingekufanya uamini kwa moyo wako wote? [Dada huyo anasema, "Amina."—Mh.] Itakufanya uamini.

Je, ingelifanya kusanyiko liamini kwa moyo wao wote?

Sasa, kila nafsi humu ndani, chini ya udhibiti wa Roho Mtakatifu, katika Jina la Yesu Kristo.

¹⁸⁹ Na yeyote yule aliyeko, mhandisi kwenye maikrofoni hizi, kama sauti yangu ikipungua, maana sijui ninalosema, kama ikipungua, iongezee sauti, kusudi kusanyiko liweze kusikia.

Sasa, iweni na kicho sana na watulivu, tunapozungumza na mwanamke huyu kwa dakika moja tu.

Kama utasimama moja kwa moja upande huu hapa, ili niwe na hakika ya kwamba watasikia. Upande ule tu. . .

¹⁹⁰ Sasa, Bwana wetu, alipomjia yule mwanamke Msamaria, Yeye alisema alihitaji kupitia Samaria, kumwona yule mwanamke. Na, bila shaka, Mungu, Baba, alikuwa amemtuma huko juu. Basi akakutana na huyo mwanamke, wala hakujuua lolote kumhusu, kamwe hakuwahi kumwona maishani Mwake, huyo mwanamke hakuwa amewahi kumwona, lakini hata hivyo, ilimbidi kumpa mwanamke huyo Msamaria ishara ile ile aliyompa Myahudi.

¹⁹¹ Na sasa wewe ni mwanamke wa Mataifa. Unaona? Sasa, Yeye hana budi kuwa ni Yesu yeye yule, jana, leo, hata milele. Hiyo ni kweli? Sasa, kama angefanya jambo kama hilo, unajua basi itabidi itoke kwa Roho fulani, unajua ingebidi iwe ni Roho. Sasa, ungeweza kuchukua upande wa Farisayo, wa kidini wa siku hiyo, na kusema ilikuwa ni ibilisi, basi hiyo ni juu yako na Mungu. Lakini kama ungesema ilikuwa ni Kristo, basi unapokea thawabu Yake.

¹⁹² Sasa, kama Roho Mtakatifu ataniambia, sasa nasema, kama ningekuja hapa na kusema, "Dada, nina karama ya uponyaji." Niweke mikono yangu juu yako, na kusema, "Utukufu kwa Mungu, Biblia inasema, 'Ishara hizi zitafuatana na hao, amini, weka mikono juu ya wagonjwa, watapata afya.'" Hiyo ni kweli. Vema, ungeweza kwenda kuamini hilo, hilo lingekuwa sawa.

¹⁹³ Lakini hata hivyo, kunaweza kuwa na tashwishi kidogo niani mwako, "Sijui kama hiyo ni kweli, kwa sababu Biblia ilisema, 'Akiwepo mmoja miongoni mwenu, aliye wa kiroho, ama nabii, yale asemayo yakitimia, basi msikieni, bali yasipotimia, basi msimsikie.'"

¹⁹⁴ Sasa, shindano la kuamua liko hapa sasa: Je, nimesema kweli? Hilo ni Neno la Mungu? Je, hiyo ni ahadi ya Mungu? Kama ndivyo, basi Yeye atalidhihirisha.

¹⁹⁵ Sasa, mwanamke huyo anajua ya kwamba yuko katika Uwepo wa Mtu fulani mbali na mwanadamu, hisia nzuri sana, nyenyekevu. Hiyo ni kweli? Kama ndivyo ilivyo, inua tu mkono wako, ili kusa-. . . Kati yangu na huyu mwanamke ni yule

Roho wa Kristo, ile Nuru. Mwanamke huyo yuko hapa apate kuombewa, kwa sababu ya ugonjwa wa wasiwasi, ana ugonjwa mbaya sana wa neva. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Unaamini?

¹⁹⁶ Hatimaye, sijawahi kuona usiku wa kwanza ila utakaofanya hivyo. Mtu fulani moyoni mwako, usifikiri unaweza kuficha mawazo yako sasa, maana huwezi, ulisema nilibahatisha hilo. Sikubahatisha. Ninii tu, ili kukukemea, upate kujua, tutaona kama ndivyo, ama sivyo. Mnaona? Kila wakati, usiku wa kwanza, wakati jambo fulani linaposemwa... Sasa, sasa hivi, nisingeweza kuwaambia yale niliyomwambia huyu mwanamke, bali mpate kujua ya kwamba ni Roho wa Mungu, wala si yale unayowazia, hili litakuwa kemeo dhahiri kwako!

¹⁹⁷ Wewe ni mtu mzuri, mtu mwenye roho nzuri, lakini sasa, naam, hili hapa linakuja tena. Huyu mwanamke anaondoka kwangu, naye ana—anasumbuliwa na ugonjwa wa wasiwasi, na ugonjwa wa matumbo. Hiyo ni kweli.

¹⁹⁸ Hebu niwaonyeshe kama mnaamini mimi ni... mtumishi wa Bwana, au la. Mwanamke huyo anayeketi papo hapo mwishoni mwa hicho kiti anasumbuliwa na ugonjwa wa matumbo, pia. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako, mama. Hiyo ni kweli. Um-hum. Unawaona hao pepo wakijaribu kulikwepa? Hawawezi kufanya hivyo. Yote yamekwisha kwako, mama.

¹⁹⁹ Una ugonjwa wa tumbo, ni kweli, tumbo lenye wasiwasi. Hapa, mpate kujua, kuniamini mimi kuwa ni mtumishi wa Mungu, nikisimama hapa chini ya upako huu, mumeo, yupo hapa, pia, ana tumbo lenye wasiwasi pia. Wewe hutoki katika jimbo hili, wala mji huu, unatoka Kansas. Unaamini Mungu anajua wewe ni nani? Bibi Walton. Sasa rudi nyumbani, umeponywa, wewe na mumeo, pia. Unaweza kwenda nyumbani ukaponywe, katika Jina la Yesu Kristo.

Sasa, unaamini sasa? Ningeweza kubahatisha hilo? Chochote kile?

Na tuinamishe tu vichwa vyetu katika ibada.

²⁰⁰ Baba yetu wa Mbinguni, tunakushukuru, katikati ya kila namna ya kitu Wewe ungali unasogea juu ya mawimbi, Wewe ni Mungu, kamwe hushindwi. Ninaomba ya kwamba utawabariki watu hawa sasa. Amina.

²⁰¹ Vema, mama hapa. Je, unaamini ya kwamba mambo haya yanayotendeka yanatokana na Roho wa Mungu, unaamini, mama? Basi sisi, tukiwa hatufahamiani, basi kama jambo fulani lingetu-... hayana budi kutukia, ambayo ingebidi yanijulishe jambo fulani kukuhusu. Na kama Mungu anaweza kusema kile umekuwa, hakika Yeye anaweza kusema kile utakachokuwa. Kama anajua ninii—kama anajua yaliyopita, anajua ya usoni, hilo linalifanya lithibitishe kwamba ni Mungu. Nanyi mnajua

ya kwamba nisingejua lolote kuhusu hilo, kwa sababu mimi ni mwanadamu tu hapa, ndugu yenu. Hiyo ni kweli.

202 Kuna imani kuu katika kusanyiko usiku wa leo, kwanza kabisa. Iliniacha ikaenda kwenye kusanyiko.

203 Ulifurahia sana uponyaji wako dakika chache zilizopita, wewe weka mkono wako juu ya mwanamke huyo, aliyeketi karibu nawe, naam, ukiwa na uvimbe huo kwenye titi lako. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Je, hatufahamiani? Punga mkono wako mbele na nyuma.

204 Ninataka kuwaulizeni jambo fulani. Aligusa nini? Yuko futi ishirini kutoka kwangu. Alifanya nini? Alimgusa Kuhani Mkuu. Mnaona ya kwamba Mungu angali anaishi? Ni Bwana Yesu yeye yule. Aminini tu. Mungu awabariki.

205 Ninaweza tu kunena kama inavyonena kupitia kwangu. Sina budi, popote iendapo, sina budi kuambatana nayo, kuninii . . . Mnaona?

206 Una uvimbe kwenye titi, una ugonjwa wa tumbo, pia. Pia, una mtu hapa ambaye ni mgonjwa, pia, mume wako. Yeye ana ninii, yeye ni mhubiri, naye ana tumbo lenye wasiwasi. Bibi Suey, rudi nyumbani ukaponywe, nyote wawili, na mponywe katika Jina la Yesu Kristo.

207 Amini, usiwe na shaka, amini tu. Unaamini ya kwamba Yesu Kristo . . . ? “Mabwana, sisi tunataka kumwona Yesu.” Huyu ni Yeye. Unaona? Huyu ni—huyo ni Bwana Yesu. Sasa, hamna budi kusema ni kitu *fulani*, mnajua hilo. Watu hawa walioinua mikono yao mbele za Mungu, hatujawahi kukutana, bali ni Roho Wake anayefanya mambo haya. Aminini tu.

208 Wewe ndiye yule mama sasa? Hatufahamiani, nadhani, lakini Bwana Yesu anatujua sote wawili. Lakini kama anaweza kunifunulia jambo fulani kukuhusu wewe, ambalo unajua kwamba silijui, ingekutia moyo kukufanya uwe na imani ya kuamini?

209 Mnaona kile Hilo linachonifanyia, linanidhoofisha sana hata ni vigumu kusimama, tunatambua hilo. Nina hakika ya kwamba kusanyiko linatambua hilo, pia. Ni wangapi wanaojua ya kwamba hilo . . . ? Kama ono moja lilimfanya Bwana wetu ahisi nguvu zikimtoka, Mwana wa Mungu, lingenifanyia nini mimi, mwenye dhambi, aliyeokolewa kwa neema? Kwa sababu Yeye alisema, “Kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya, *nyingi* kuliko hizi mtazifanya.” Sasa, ninajua King James linasema *kubwa* zaidi, lakini lifuatilieni kwenye ile tafsiri ya asili, mnaona. Ungewezaje kufanya makubwa zaidi? Alikomesha maumbile, akafufua wafu, akafanya kila kitu ambacho kingeweza kufanywa, lakini *nyingi* zaidi, kwa sababu Yeye angeweza kuwa katika Kanisa Lake la ulimwenguni kote. Mnaona? “Nyingi kuliko hizi mtafanya.” Ni neema Yake.

210 Uko hapa kwa ajili ya mtu mwingine, huyo ni binti. Unafikiri Kristo anaweza kuniambia shida yake ni nini? Ni macho yake. Hiyo ni kweli, sivyo? Unaamini yatapona sasa? Umewasiliana na Kitu fulani, sivyo? Unaamini Hicho kuwa ni Bwana Yesu? Kama ataniambia wewe ni nani, kama alivyomwambia yule mtume aliyekuja, ungeninii... kukufanya uwe na imani nyingi kumwamini Yeye? Vema, Bibi Nickels, wewe rudi nyumbani, amini sasa, Yesu Kristo ataponya na kukupa afya.

Mnaamini, kila mtu? Tafadhalini msitembee-tembee. Tafadhalini msitembee-tembee, tafadhalini.

211 Sikujui wewe. Sijapata, sijawahi kukuona maishani mwangu, bali Kristo anakujua. Kama atanielezea kile kilichokuleta hapa, ama, huenda ikawa ni fedha, mambo ya nyumbani, huenda ikawa ni ugonjwa, wokovu; sijui, mimi ni mtu tu aliyesimama hapa, tukikutana kwa mara ya kwanza maishani.

212 Jambo moja, una wasiwasi kweli. Hiyo ni kweli. Nami ninakuona ukijaribu kutoka kitandani, polepole sana. Una yabisi kavu. Hiyo ni kweli. Halafu basi, una matokeo mabaya, athari mbaya kutokana na upasuaji uliofanyiwa. Hiyo ni kweli. Ilikuwa ni upasuaji wa kibofu nyongo. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Unaamini sasa? Basi nenda, kama ulivyoamini, ndivyo itakavyokuwa kwako.

Kama ningekwambia ya kwamba Mungu aliponya yabisi kavu, ungeamini ilimaanisha wewe? Basi endelea mbele tu moja kwa moja ukimshukuru Mungu, ukisema, "Asante, Bwana."

Kama nilikwambia Mungu aliponya kutokana na ugonjwa wa anemia, ungeamini ya kwamba angekuponya? Endelea tu kumshukuru Mungu, ukiamini kwa moyo wako wote.

Mnaamini kwa mioyo yenu yote, kila mtu, kwa nia moja?

213 Vipi kama sikusema neno moja kwako, nikaweka tu mikono juu yako, ungeamini? Vema, bwana. Pita, na katika Jina la Bwana Yesu, nenda ukaponywe, nenda. Usiwe na shaka, ku-...

214 Tafadhalini msitembee-tembee. Mnaona, inamhuzunisha Roho aniondokee, wala kamwe siwezi kumzuia. Mnaona? Tafadhalini, tafadhalini, nawaomba kwa wema, kama ndugu Mkristo. Niliwaomba kama hamkuamini, "Tafadhalini msikae humu jengoni." Ni hatari kwenu kukaa kwa vyovyote vile. Mnaona? Iweni tu na imani. Msitie shaka.

215 Kama nilikuwekea mikono, ungeamini ya kwamba ungepona? [Ndugu huyo anasema, "Naam, bwana."—Mh.] Njoo hapa. Katika Jina la Yesu Kristo, ndugu yetu na aponywe.

216 Njoo. Kama nilikwambia shida yako au la, ungeniamini kama nabii Wake, ama, mtumishi Wake? Vema, ugonjwa wako wa mgongo umekwisha. Nenda, na uamini sasa. Mwamini Mungu.

217 Njoo, mama. Kama sikusema neno moja kwako, bali nilikuwekea tu mikono, ungeamini kwa vyovyote vile? Vema, nataka kukwambia, ulipokuwa mstarini, ukisimama pale chini, ukaingia mstarini, uliona jambo hilo la kwanza likitukia, ugonjwa wa moyo ulikuacha, kwa hiyo unaweza kwenda nyumbani sasa. Naam, bwana.

Unatembea tofauti tangu ulipoingia mle, sivyo? Yabisi kavu ilikuacha mstarini, kwa hiyo nenda tu ukiamini kwa moyo wako wote.

218 Dada, bila shaka, moja ya shida zako kuu, sote tunajua, lakini hili ni jambo moja, kuna yapata asilimia tisini na tano ya kusanyiko hili linalougua kitu kile kile, ugonjwa wa fadhaa. Una wasiwasi sana, hiyo si ni kweli? Hebu nikunyoeshe jinsi ingekuwa vigumu kuwaita. Kila mtu anayeugua ugonjwa wa wasiwasi, inueni mikono yenu, huko nje. Unaona? Unaona pale? Umejaribu kupata mahali pa kuanzia, walikwambia, rudia fahamu zako, Shetani alikwambia utarukwa na akili, na mambo haya yote, bali ni uongo. Unaamini kwa moyo wako wote? [Dada huyo anasema, "Ninaamini."—Mh.] Basi kutoka papa hapa, katika Jina la Yesu Kristo, nenda, na uwe mzima kwa ajili ya utukufu wa Mungu.

Kama unaweza kuamini!

219 Mtu huyo ameketi pale akilia kwa muda kidogo, akiniangalia, una shida kifuari. Unaamini ya kwamba Mungu Mwenyezi atakuponya? Kama unaamini, unaweza kuupokea, bwana. Inua mikono yako, likubali, nenda nyumbani, na upate afya.

Yabisi kavu yako imekwisha. Nenda nyumbani, ukaponywe katika Jina la Yesu Kristo. Mungu akubariki.

220 Mama mmoja ndio kwanza ainue mkono wake juu, pale, akauweka nyuma ya kichwa chake, akiwa na ugonjwa wa ngozi, unaamini ya kwamba Mungu atakuponya? Una kadi ya maombi? Huna? Huhitaji yoyote, umeponywa kwa vyovyote vile. Yesu Kristo anakuponya na kukupa afya.

221 Je, ninyi waaminio, kila mmoja wenu huko nje sasa, mnamwamini Mwana wa Mungu kwa uchaji? Unaamini ya kwamba ni Roho Wake hapa? Na kama akifanya hivyo, anatimiza Neno Lake... Unasema, "Ndugu Branham, waweza kuniponya?" La, siwezi kufanya hivyo, Yeye tayari amelifanya. Mnaona? Ni jambo ambalo Yeye amefanya. Yeye yupo tu hapa, Yeye... Kama angekuwa amesimama hapa amevaa suti hii, asingeweza kukuponya, maana Yeye tayari amefanya jambo hilo, Yeye angesema, "Hivi hutaamini?" Anajitambulisha tu kwamba Yeye yupo hapa. Ni wangapi wanaoamini kwa mioyo yenu yote?

222 Sasa, nitawapa jambo la kufanya kusudi kila mtu hapa aponywe. Ni waaminio wangapi, mnasema walikuwako? Inueni mikono yenu, kotekote, kila mahali. Yesu alisema, agizo Lake

la mwisho kwa Kanisa Lake, agizo Lake la kwanza lilikuwa, “Enendeni mkawaponye wagonjwa, mkawafufue wafu, mkatoe pepo,” agizo Lake la mwisho lilikuwa, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio, katika Jina Langu watatoa pepo, watasema kwa lugha mpya. Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya.” Hiyo ni kweli?

²²³ Sasa, kila mmoja wenu kama waaminio, mwekee mkono mtu aliye karibu nawe. Weka tu mkono wako popote ulipo, weka tu mkono wako, kama wewe ni mwaminio. Mna haki ya kuwekeana mikono ninyi kwa ninyi, kama tu mtu mwingine yeyote alivyo nayo.

²²⁴ Sasa, usijiombe mwenyewe, kwa sababu mtu uliyemwekea mikono yako anakuombea. Mwombe mtu mwingine, watakuwa wakikuombea. Nami nitawaombea kutoka kwenye jukwaa hili, naye Mungu wa Mbinguni, aliyemfufua Yesu katika wafu, na kumfanya hai milele, Yeye yupo hapa usiku wa leo, kutimiza kila Neno alilosema. Ni Uwepo Wake.

²²⁵ Sasa, wewe inamisha kichwa chako ninapokuombea. Na uamini tu kwa moyo wako wote kwamba Mungu atayasikia maombi yangu. Hakika mnafahamu ya kwamba si mimi, ni Roho Mtakatifu sasa amethibitisha Neno la Mungu kuwa kweli.

²²⁶ Kabla tu hatujaomba, huku vichwa vyenu vimeinamishwa, kama kuna asiyeamini, alikuwa, humu ndani, na sasa ni mwaminio, waweza kusimama kwa miguu yako upate kutambuliwa katika maombi, tunapomba? Mtu fulani anayetaka kumpokea Kristo kama Mwokozi binafsi, waweza kusimama kwa miguu yako upate kukumbukwa katika maombi sasa hivi, wakati ukiwa katika Uwepo Wake wa Kiungu? Je, kungeweza kuwa na wale hapa, ambao wangependa kumkubali sasa hivi, waweza kusimama kwa miguu yako?

²²⁷ “Yeye atakayenishuhudia Mimi mbele ya watu, huyo nitamshuhudia mbele za Baba Yangu, na Malaika watakatifu.”

²²⁸ Simama sasa hivi, na useme, “Nitamkubali Yesu Kristo kama Mwokozi Wangu. Uko hapa, nami najua hilo, lakini, amekufunulia Wewe.” Lakini usitegemee ufuasi wa kanisa lako, kwa sababu haufai kitu. Huna budi kumpokea Roho Mtakatifu, la sivyo umekwisha. Sasa, kumbukeni, si mimi, ni Roho Mtakatifu anayetimiza Neno Lake. Kwa hiyo ukitaka kusimama, simama sasa, tunapomba.

²²⁹ Baba yetu wa Mbinguni, hizi ndizo saa za kuimalizia historia ya ulimwengu huu. Tunajua ya kwamba hakuna tiba iliyosalia, Kuja kwa Mwana wa Mungu kumekaribia. Yeye alisema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Sodom, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu.” Tunaona mabomu ya atomiki na mabomu ya haidrojeni, na kila taifa dogo, likingojea tu mtu fulani aachilie moja, kisha hiyo iingie katikati ya hewa, huko ng'ambo, kama ju—jua likitokeza, dunia hii itatoweka.

Lakini kabla hilo halijatukia... Nasi tunajua huenda ikawa ni kabla ya asubuhi, huenda ikawa ni dakika yoyote. Kama vile mwanasayansi wetu anavyotwambia, ni muda mrefu uliopita, dakika tatu ifike usiku wa manane. Lakini tunajua mkono wa Mungu umeusimamisha wakati, kungojea, uvumilivu tu, kama alivyokuwa katika siku za Nuhu.

²³⁰ Na sasa, umethibitisha jambo Lako la mwisho ulilosema ungefanya kabla tu ya Sodoma kuteketezwa, mara baada ya ishara hiyo kumalizika, Sodoma iliteketezwa. Mungu, karibu imekwisha. Lakini kuna Mtu Mmoja tu anayeweza kuivuta mioyo ya watu, Wewe ulisema, “Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu, asipovutwa na Baba Yangu kwanza.” Wengi wataona, na kusikia, na kutembea daima gizani, waliokusudiwa hukumumu hii, kama vile Kitabu cha Yuda kilivyosema. Akili potovu, nafsi zinazotangatanga kama nyota zilizopotea, mawimbi ya bahari yasiyozuilika, yakitoa aibu yao wenyewe kama povu la kutokuamini.

²³¹ Kujua, usiku wa leo, ya kwamba tunasimama Mbele ya Roho Mtakatifu mkuu, Yule aliyelileta Neno, Ambaye aliliandika Neno, Ambaye hulithibitisha Neno, na kuleta Uwepo Wake Mwenyewe, kutimiza Neno ambalo Yeye ameahidi, ninawaomba hawa waaminio, ambao wamewekeana mikono, ninaomba kwa moyo wangu wote ya kwamba utaiponya miili yao iliyo migonjwa, utoe kila pepo mchafu.

²³² Shetani, umeshindwa vi—vita, wewe ni mtu aliyeshindwa, huna haki tena.

²³³ Bwana wetu Yesu alikufa pale Kalvari, na kwa Damu Yake takatifu, isiyoghoshiwa, Damu ya Mwenyezi Mungu iliyovunjwa pale Kalvari, Wewe uliikomboa jamii ya binadamu, Bwana. Nawe ukamshinda Shetani kwa Damu iyo hiyo, ukamvua kila nguvu aliyokuwa nayo. Nawe u hai usiku wa leo, hapa Bloomington, Illinois, katika uwanja huu wa mpira wa chuo, uko hapa usiku wa leo, u hai miongoni mwa watu Wako, ukijithibitisha Mwenyewe, ya kwamba Wewe ni yule yule jana, leo, na hata milele, naye Shetani anajua hilo, anajua ya kwamba saa yake imekaribia.

²³⁴ Shetani, ninakuapisha kwa Mungu aliye hai, tunakemea udanganyifu wako, huwezi kuwashikilia watu hawa wagonjwa tena, toka ndani yao, katika Jina la Yesu Kristo, uwaondokee na uwaache! Bwana Mungu wa Mbinguni na akukemee, ewe Shetani! Huwezi kuwa na nguvu zozote, Yesu yuko juu yako, alikunyang'anya hizo nguvu, aliikomboa jamii ya binadamu imrudie Yeye. Toka, ninakuapisha, kwa Mungu aliye hai, kwamba uwaondokee watu hawa!

²³⁵ Sasa, wakati mmewekeana mikono, jinsi mnavyoomba kanisani mwenu wenyewe, weka mikono yako juu ya mtu aliye karibu nawe, na kuwaomba, ombeni tu jinsi mnavyoomba

kanisani mwenu. Weka mikono yako juu ya mtu fulani, na mwombeane. Ndipo ukihisi imani ya Mungu aliye hai, Yeye aliyepo sasa, ikimiminika nafsini mwako kukufanya mwaminio, basi inuka katika Jina la Yesu Kristo, na kudai uponyaji wako kwa ajili ya utukufu wa Mungu. 

61-0409 Mabwana, Sisi Tunataka Kumwona Yesu
Illinois Wesleyan University
Bloomington, Illinois Marekani

SWAHILI

©2025 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org